BENKI YA BIASHARA MKOMBOZI

# MKUTANO MKUU WA 17 WA WANAHISA

25 JULAI, 2026

# BODI YA WAKURUGENZI



Bw. Gasper Njuu
Mwenyekiti wa Bodi



Bw. Respige Kimati
Mkurugenzi Mtendaji



Bw. Benedict Sudi
Mjumbe



Bi. Uphoo Swai
Mjumbe (Mstaafu)



Askofu Mkuu. Beatus Kinyaiya
Mjumbe



Bw. Robert Mtendamema
Mjumbe (Mstaafu)



Padre Dkt. Charles Kitima
Mjumbe



Bw. Damas Damiani Mugashe
Mjumbe



Bw. Martin Mdoe
Mjumbe



Bi. Agnes Charles Kitwanga
Mjumbe

# TIMU YA UENDESHAJI



Bw. Respige Kimati
Mkurugenzi Mtendaji



Bw. Vitalis Michael
Afisa Mkuu wa Fedha



Bw. Leonard John
Afisa Mkuu wa Operesheni



Bw. Crispin Kweka
Mkaguzi Mkuu wa Ndani



Bi. Paulina Kunjumu
Mkuu wa Idara ya Sheria



Bw. Wilbert Luoga
Mkuu wa Idara ya Mkopo



Bi. Fortunata Olomi
Afisa Mkuu wa Biashara



Bi. Stella Shangali
Mkuu wa Idara ya
Rasirimali Watu



Bw. Daudi Senkondo
Mkuu wa idara
Ukubalifu na
Vihatarishi



Bw. Faraja Augustino
Mkuu wa Hazina

# YALIYOMO


1. Dira ........................................................ 1

2. Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Mwaka........................................2

3. Taarifa ya Mwenyekiti ........................................4

4. Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji ........................................8

5. Dondoo za Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kumi na Sita..................11

6. Yatokanayo na Dondoo za Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kumi na Sita........................................38

7. Taarifa ya Wakurugenzi ........................................42

8. Taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu wa Nje na Taarifa za Fedha ...........60

9. Pendekezo la kutoa Gawio kwa mwaka 2025........................................91

10. Uteuzi wa Mkaguzi Mkuu wa Nje........................................91

11. Pendekezo la kufanya mapitio ya malipo ya Wakurugenzi..............91

12. Tarehe na Mahali utakapofanyika Mkutano Mkuu ujao........................92





# DIRA NA DHIMA

## DIRA

Kuwa benki inayoongoza katika kushughulikia mahitaji ya ukuaji wa biashara ndogo na za kati kwa kutoa huduma za kibenki zenye viwango vya hali ya juu na kwa uadilifu kwa wateja wote kuanzia wadogo kabisa na kampuni za biashara.

## DHIMA

Kuwa benki itakayotoa huduma za kifedha za viwango vya juu kwa sekta zote na viwango vyote vya uchumi kwa namna ambayo ni endelevu huku ikiwajibika kwa jamii ili kukidhi matarajio ya wadau..



# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA

**Taarifa inatolewa kuwa** Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa wa Benki ya Biashara Mkombozi utafanyika tarehe **25 Julai, 2026** kuanzia **saa tatu kamili asubuhi** katika ukumbi wa jengo la PSSSF Commercial Complex lililopo Barabara ya Sam Nujoma, Ubungo, Dar es Salaam.

## AJENDA

1. Kuthibitisha akidi na Kufungua Mkutano;
2. Kupitishwa kwa Ajenda ya Mkutano;
3. Kuthibitisha dondoo za Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 16 uliofanyika 26 Julai, 2025;
4. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 16 uliofanyika 26 Julai, 2025;
5. Kupokea, kujadili na kuidhinisha Taarifa ya Wakurugenzi ya mwaka ulioishia 31 Desemba, 2025;
6. Kupokea, kujadili na kuidhinisha Taarifa za Fedha za Benki kwa mwaka ulioishia 31 Desemba, 2025 pamoja na kupokea taarifa ya Mkaguzi wa Nje wa hesabu juu ya taarifa hiyo ya fedha;
7. Kupokea, kujadili na kuidhinisha pendekezo la Gawio kwa Mwaka 2025;
8. Kuteua Mkaguzi wa nje wa hesabu za Benki;
9. Kupokea, kujadili na kuidhinisha viwango vya malipo ya Wakurugenzi;
10. Kupanga tarehe ya Mkutano Mkuu wa Mwaka ujao;
11. Mengineyo, na;
12. Kufunga Mkutano.

## MAELEZO:

1. Mwanahisa anayetarajia kuhudhuria Mkutano Mkuu wa mwaka anapaswa kuwa na namba ya CDS kama inavyoonekana katika Hati ya Uwekezaji wa Hisa na kitambulisho halali.

2. Mwanahisa mwenye stahili ya kuhudhuria mkutano huu ana haki ya kumteua mwakilishi wake wa kupiga kura kwa niaba yake kwa mujibu wa taratibu za kampuni. Fomu husika inayopaswa kujazwa na Mwanahisa kwa ajili ya uteuzi huo inatakiwa kufikishwa kwa katibu wa Benki siku tatu kabla ya mkutano. Kwa taasisi, fomu inapaswa kuwa katika lakiri ya taasisi ya Mwanahisa. Fomu hiyo iandikwe kama ifuatavyo.

**"Benki ya Biashara Mkombozi"**

Benki ya Biashara Mkombozi Mimi/Sisi.....................................................................................wa............................ ..............................................., nikiwa/tukiwa Mjumbe/Mwanahisa wa kampuni iliyotajwa hapo juu, ninamteua/tunamteua ....................... .................................. wa ............................................................ .............. ........................... kama mwakilishi wangu/wetu kupiga kura kwa niaba yangu/yetu katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa wa Benki utakaofanyika terehe 25 Julai, 2026.

Saini ......................................................... Imetolewa leo tarehe..................Mwezi....................2026.

3. Wanahisa wote na/au wawakilishi wao watahitajika kujisajili kwanza kabla ya kuingia kwenye ukumbi siku ya mkutano.

4. Vitabu vyote vilivyo na ripoti za kifedha na taarifa nyingine muhimu za benki vitapatikana kwenye matawi ya Benki na tovuti ya Benki https://mkombozibank.co.tz/ wiki tatu kabla ya mkutano.

Kwa maelezo na taarifa zaidi, wasiliana na Ofisi ya Benki kwa anuani ifuatayo:
Benki ya Biashara Mkombozi,
Kiwanja Namba 40, Nyuma ya Kanisa la Mtakatifu Yosefu,
Mtaa wa Mansfield,
S.L.P 38448,
DAR ES SALAAM.
Namba za Simu: +255 22 2137806/7.
Namba ya bure ya maulizo: 0800 750 040
Barua Pepe: shareholders@mkombozibank.co.tz
info@mkombozibank.co.tz
Web:www.mkombozibank.co.tz

**PAULINA KUNJUMU**
**KATIBU NA MWANASHERIA WA BENKI**
**KWA AMRI YA BODI YA WAKURUGENZI**
**JUNI,2026.**

# TAARIFA YA MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI WA BENKI

## Utangulizi

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, ninatumia fursa hii kuwakaribisheni nyote katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kumi na Saba wa wanahisa wa Benki ya Biashara Mkombozi. Ninaona fahari kuwasilisha kwenu mambo muhimu ya Ripoti ya Mwaka na Taarifa ya Fedha ya Benki kwa mwaka ulioishia Desemba, 2025

Ninaipongeza Menejimenti ya Benki pamoja na wafanyakazi wote kwa kufanya kazi kwa bidii na kuwezesha kupatikana mafanikio yaliyoainishwa katika Ripoti hii. Vilevile, ninawashukuru wenzangu, wajumbe wa Bodi kwa kutoa miongozo na uangalizi bora uliofanikisha utekelezaji wa malengo ya Benki. Leo hii ninasimama mbele yenu na kuwasilisha kwenu mafanikio ya Benki kwa mwaka 2025 kutokana na kujitolea bila kuchoka na mchango wa kila mmoja wetu katika kufanikisha malengo ya Benki.

Kwa dhati kabisa, ninawashukuru wateja wetu kwa kuendelea kuiunga mkono Benki yetu. Bila wao, Benki isingeweza kuyafikia mafanikio haya. Ninatumia pia fursa hii kuzishukuru taasisi zinazosimamia na kudhibiti sekta ya fedha ambazo ni pamoja na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Serikali na wadau wengine wote ambao kwa namna moja au nyingine wamekuwa wakiunga mkono na kutoa mwongozo kwa Benki. Kwa wanahisa wetu, ninawashukuru sana kwa kuendelea kuunga mkono na kuwezesha upatikanaji wa rasilimali mtaji ili kufanikisha malengo ya Benki.

## Mafanikio na Maendeleo Makuu ya mwaka 2025.

Wakati matokeo ya utendaji wetu yameainishwa katika kurasa 62-90, yanayoonesha ukuaji wa biashara yetu, nawaomba mpitie pia maendeleo muhimu yafuatayo na kusoma Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji katika Ripoti hii ya Mwaka, ambayo inatoa maelezo ya kina kuhusu biashara yetu na mipango ya baadaye.

- Tumeanzisha na kusambaza suluhisho la usimamizi wa fedha kwa shule na hospitali ili kuimarisha ukuaji wa biashara kupitia amana na mapato ya miamala.

- Tumeendelea kupanua mtandao wa matawi kwa kufungua tawi jipya la Geita, hivyo kufikisha jumla ya matawi 14, na kukamilisha maandalizi ya awali ya matawi mengine manne yatakayofunguliwa mwaka 2026 katika maeneo ya Kahama, Bagamoyo, Same na Mbeya.

- Tumeanzisha mpango mkakati maalumu kwa wateja wote wenye akaunti na benki unaolenga kupata biashara kubwa kutoka kwao kwa lengo la kuongeza sehemu ya huduma wanazotumia benki kupitia mauzo ya ziada na huduma zinazokamilishana pamoja na kuimarisha mnyororo wa thamani ili kupanua mizania ya benki.

- Tumeimarisha mkakati wa kuvutia na kuhudumia wateja wetu wa kimkakati kwa kutumia suluhisho za kidijitali pamoja na bidhaa/huduma zilizoboreshwa kulenga mahitaji ya wateja wetu.

Kwa ujumla, juhudi za kuimarisha na kukuza biashara zetu zimeendelea kuzaa matunda kupitia ongezeko la wateja, mapato, usimamizi bora wa gharama na udhibiti thabiti wa vihatarishi.

**Hali ya Uchumi na Sdko mwaka 2025.**

Uchumi wa Tanzania kwa mwaka 2025 umekua kwa 5.9% kutoka 5.6% mwaka 2024. Ukuaji huu umechangiwa zaidi na sekta za kilimo, madini na ujenzi. Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2025 unakadiriwa kukua kwa 6.8%, ukichochewa na sekta za ujenzi, utalii na viwanda. Mtazamo wa muda wa kati ni chanya, ambapo ukuaji wa Pato la Taifa unatarajiwa kubaki imara katika kiwango cha takriban 6% kwa Tanzania Bara na 7.2% kwa Zanzibar.

Mfumuko wa bei umeendelea kuwa wa chini na thabiti, ukibaki ndani ya lengo la 3%–5%. Wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa 3.4% mwaka 2025 kutoka 3.1% mwaka 2024. Hali hii ilichangiwa na sera madhubuti ya fedha na mazingira mazuri ya kimataifa yaliyosaidia kuimarika kwa shilingi na kupunguza mfumuko wa bei unaotokana na bidhaa zinazoagizwa nje. Matarajio ni kuwa mfumuko wa bei utaendelea kubaki ndani ya lengo la 3% hadi 5% mwaka 2026.

Katika kipindi kijacho, mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki tulivu katika uchumi mbalimbali, hali itakayosaidia mazingira thabiti ya bei nchini Tanzania. Hata hivyo, mvutano wa kisiasa duniani hasa Mashariki ya Kati umeongeza kutokuwa na uhakika katika masoko ya nishati

na bidhaa. Hivyo bei ya mafuta ghafi, ambayo kwa sasa ipo juu ya makadirio ya Dola za Marekani 62–65 kwa pipa, inaweza kubaki juu au kupanda zaidi kutegemea muda na ukubwa wa migogoro, usumbufu wa minyororo ya usambazaji, na maamuzi ya Shirikisho la Wazalishaji Wakubwa wa Nishati ya Mafuta Duniani ("OPEC+").

Mwaka 2025, utekelezaji wa sera ya fedha ulikuwa wa kuridhisha, ambapo ukwasi wa uchumi uliendana na hali ya shughuli za kiuchumi. Sera hiyo ilitekelezwa kupitia mikopo ya repo na reverse repo, dhamana za serikali za siku 35, 91 na 182, pamoja na shughuli za fedha za kigeni. Benki pia zilisawazisha nafasi za ukwasi kupitia dirisha la mikopo la Benki Kuu ya Tanzania (BOT). Mwaka 2026, sera ya fedha itaendelea kuwa nyenzo muhimu katika kudhibiti shinikizo la mfumuko wa bei.

Upatikanaji wa fedha (money supply) uliendelea kukua kwa kasi na kwa uthabiti, sambamba na sera ya fedha na kasi ya ukuaji wa uchumi. Kutokana na sera ya fedha iliyokuwa rafiki kwa uchumi, kiwango cha fedha msingi kiliongezeka kwa 26.2% mwaka 2025 kutoka 19.1% mwaka 2024. Huku kizidishi cha fedha kikibaki thabiti, fedha pana (M3) ilikadiriwa kukua kwa 24.6% mwaka 2025 kutoka 11.1% mwaka 2024. Ukuaji huo ulisukumwa zaidi na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi kutokana na kuongezeka kwa amana za sarafu ya shilingi.

Mikopo kwa sekta binafsi iliendelea kukua kwa kasi katika mwaka 2025, ambapo kiwango cha mikopo kilifikia takriban TZS trilioni 43.4 kufikia Desemba 2025, sawa na 21% ya Pato la Taifa, kutoka 17.4% mwaka uliotangulia. Mwenendo huu ulikuwa sambamba na nchi nyingi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Africa (SADC). Viwango vya riba za mikopo vilikuwa kati ya 15% hadi 16%, wakati riba za amana zilikuwa karibu 8%. Riba za mikopo kwa makubaliano maalumu kwa wateja wakubwa zilikuwa takriban 12% kutoka 10% mwaka 2024, huku riba za amana za makubaliano maalumu zikifikia wastani wa 11% kutoka 10% mwaka 2024. Hata hivyo, viwango hivi vilibaki chini ukilinganisha na nchi nyingi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

### Mpango Mkakati wa 2025–2026

Benki inaendelea kutekeleza mikakati ya muda mfupi na wa kati kwa lengo la kupata faida endelevu, ukuaji wa biashara na faida kwa wanahisa kupitia mgao wa faida. Tutaendelea kupenya sokoni kwa kutoa suluhisho bora za kifedha na kutumia kikamilifu fursa zilizopo ndani ya soko letu la kimkakati.

## Nyaraka za Mkutano Mkuu wa Mwaka

Nyaraka za Mkutano Mkuu wa Mwaka, ambazo tayari zimewasilishwa kwa wanahisa, zinajumuisha Taarifa ya Wakurugenzi na Taarifa ya Fedha ya benki kwa mwaka ulioishia 31 Desemba 2025. Hizi zitawasilishwa rasmi kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa. Wanahisa mnakaribishwa kuchangia mawazo na mapendekezo kwa mafanikio zaidi ya benki.

Asanteni,

**GASPER CASMIR NJUU**
**MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI**
**25 JULAI 2026**



# TAARIFA YA MKURUGENZI MTENDAJI

## Utangulizi.

Nina furaha kuripoti kuwa mwaka wa fedha 2025 umekuwa wa utendaji imara kwa Benki ulioendeleza mwenendo wa ukuaji thabiti uliowekwa katika miaka iliyotangulia. Mafanikio haya yanaonesha uimara wa mwelekeo wetu wa biashara, kujituma kwa wafanyakazi wetu, na kuendelea kuaminiwa na wadau wetu.

Benki ilipata ukuaji mkubwa wa faida, amana na rasilimali, jambo linalodhihirisha dhamira yetu ya kuimarisha ufanisi wa kiutendaji, kuboresha huduma kwa wateja na utekelezaji madhubuti wa mipango yetu ya kimkakati.

## Muhtasari wa Utendaji kwa Mwaka 2025

i. Faida Kabla ya Kodi iliongezeka kwa 48% na kufikia TZS bilioni 17.00 (kutoka TZS bilioni 11.49 mwaka 2024), ongezeko lililosababishwa zaidi na kuongezeka kwa mapato na hatua za kudhibiti na kupunguza gharama.

ii. Jumla ya mali ilikua kwa 13% na kufikia TZS bilioni 318.23 (kutoka TZS bilioni 282 mwaka 2024), ikiwa imechangiwa zaidi na ukuaji wa mikopo kwa wateja.

iii. Faida kwa Hisa za Wanahisa iliongezeka kwa 34% (kutoka 29% mwaka 2024), huku mtaji wa wanahisa ukikua kwa 23% na kufikia TZS bilioni 49 (kutoka TZS bilioni 40 mwaka 2024).

iv. Mikopo kwa wateja ilikua kwa 16% na kufikia TZS bilioni 188.93 (kutoka TZS bilioni 162.57 mwaka 2024), ikichangiwa na mikakati bora ya utoaji na usimamizi wa mikopo.

v. Amana za wateja ziliongezeka kwa 12% na kufikia TZS bilioni 242.86 (kutoka TZS bilioni 217.49 mwaka 2024), huku uwiano wa akaunti za amana za kawaida na akiba ukiongezeka hadi 73% (kutoka 68% mwaka 2024). Hii ilitokana na mikakati ya kusajili wateja wapya ili kuongeza amana hususan kutoka soko letu la Kimkakati.

vi. Mapato halisi ya uendeshaji yaliongezeka kwa 26% na kufikia TZS bilioni 36.78 (kutoka TZS bilioni 29.21 mwaka 2024), yakichangiwa na ukuaji thabiti wa mapato na udhibiti mzuri wa gharama za uendeshaji.

vii. Uwiano wa gharama na mapato ulifikia 52%, ukiwa ndani ya kiwango cha kisheria cha 55%. Hii inaonesha ufanisi ulioboreshwa wa mapato na udhibiti wa gharama katika maeneo yote ya shughuli za benki.

viii. Mikopo chechefu ilikuwa 4.4%, ikiwa ndani ya kiwango cha kisheria cha 5%, kutokana na mikakati imara ya utoaji mikopo na usimamizi wa ufanisi wake.

ix. Mtandao wa mawakala wa kibenki (Wakala) uliongezeka kwa 42% na kufikia mawakala 1,957 (kutoka 1,377 mwaka 2024), ambapo 28 kati yao ni mawakala wa kimkakati waliopo katika maeneo maalum ya Parokia au Taasisi za Kanisa, ambazo ni sehemu muhimu ya soko mkakati la benki. Ukuaji huu umechangiwa na mkakati wa kulenga masoko maalumu na umeongeza upatikanaji wa huduma na ukuaji wa biashara.

x. Programu za benki kwa simu (“Mkombozi Mobile Application”), huduma ya USSD (*150*06#), pamoja na suluhisho za usimamizi wa fedha kwa taasisi kama vile “SchoolPay”, “Hospital Solution” na “Sadaka Digital” zimeendelea kutoa huduma bunifu na rahisi kwa wateja wetu mbalimbali.

xi. Benki imeendelea kupanua uwepo wake katika mikoa muhimu ya kiuchumi kwa kufungua matawi mapya kama vile Geita na Kahama mwezi Novemba 2025 na Mei 2026 mtawalia na kituo cha huduma za kibenki kilichopo Bagamoyo Juni 2026. Uwekezaji huu unaendana na mkakati wetu wa kuimarisha ukuaji wa biashara na faida endelevu.

Mafanikio haya yanaimarisha azma yetu ya kutoa huduma bora za kibenki zenye viwango vya juu vya uadilifu na ubora.

## Vipaumbele Muhimu kwa Kipindi Kijacho

- **Kuimarisha matumizi ya Teknolojia za Kidijitali:** Benki itaendelea kuwekeza katika utoaji wa suluhisho za kidijitali kwa wateja wake walengwa ili kuongeza ufanisi wa shughuli za biashara na kuboresha huduma kwa wateja.

- **Ukuaji wa Soko:** Tutaendelea kuimarisha uwepo wetu na ushirikiano na wateja katika masoko yetu maalum, sambamba na kutafuta fursa mpya za ukuaji kupitia mipango ya akaunti na usimamizi wa mahusiano na wateja.

- **Uzoefu wa Wateja:** Benki itaendelea kuboresha thamani ya huduma kwa wateja kwa lengo la kuvutia na kuhifadhi wateja wenye mchango mkubwa katika ukuaji endelevu wa biashara, huku tukihakikisha utoaji wa huduma bora zenye viwango vya juu.

- **Ujumuishaji wa Kifedha:** Tutaendelea kupanua huduma kupitia matawi ya benki na njia za kidijitali ili kuongeza upatikanaji wa bidhaa na huduma za kifedha kwa wateja wetu walengwa.

- **Watu na Utamaduni wa Kazi:** Benki itaendelea kujenga utamaduni wa utendaji wa hali ya juu na kuwawezesha wafanyakazi wake kupitia mafunzo na programu za maendeleo ya kitaaluma ili kuhakikisha ufanisi wa muda mrefu katika shughuli za benki.

### Kuongeza Thamani kwa Wanahisa

Benki inaendelea kutumia nafasi yake ya kimkakati kuimarisha utendaji na kuongeza manufaa kwa wanahisa. Matokeo mazuri ya utendaji yanaonekana kupitia ongezeko la gawio hadi TZS 100.00 kwa kila hisa mwaka 2025 kutoka TZS 92.40 kwa kila hisa mwaka mwaka 2024. Matokeo haya yanadhihirisha uwezo wetu wa kuendeleza ukuaji, kuongeza thamani ya muda mrefu kwa wanahisa, pamoja na kudumisha nidhamu katika usimamizi wa vihatarishi na mtaji.

### Shukrani

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wanahisa na wateja wetu kwa kuendelea kutuamini na kutuunga mkono. Tunaishukuru Bodi ya Wakurugenzi kwa mwongozo na ushirikiano wao endelevu. Vilevile, tunawashukuru wasimamizi wetu wa sekta kwa ushirikiano na msaada wao wa karibu.

Mwisho, lakini si kwa umuhimu, nawapongeza na kuwashukuru wafanyakazi wote kwa kujituma kwao, bidii na mchango wao mkubwa katika kufanikisha malengo yetu ya utendaji kwa mwaka 2025 na katika kujenga mustakabali bora wa taasisi hii.



**RESPIGE KIMATI**
**MKURUGENZI MTENDAJI.**
**25 JULAI, 2026.**

# DONDOO ZA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA KUMI NA SITA

## AJENDA NAMBA 3

**KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA KUMI NA SITA WA WANAHISA ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA SELOUS, KITUO CHA MIKUTANO CHA KIMATAIFA CHA JULIUS NYERERE (JNICC), POSTA, DAR ES SALAAM, SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 26 JULAI 2025.**

**MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA KUMI NA SITA WA MWAKA WA WANAHISA WA BENKI YA BIASHARA MKOMBOZI ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA SELOUS, KITUO CHA MIKUTANO CHA KIMATAIFA CHA JULIUS NYERERE (JNICC), POSTA, DAR ES SALAAM, SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 26 JULAI 2025.**

### WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Gasper Njuu | - | Mwenyekiti |
| 2. | Askofu Mkuu Beatus Kinyaiya | - | Mjumbe |
| 3. | Bw. Benedict Sudi | - | Mjumbe |
| 4. | Bw. Martin Mdoe | - | Mjumbe |
| 5. | Bw. Robert Mtendamema | - | Mjumbe |
| 6. | Bw. Respige Kimati | - | Mkurugenzi Mtendaji |
| 7. | Bi. Paulina Kunjumu | - | Katibu wa Kampuni (Mwanasheria) |

### WAJUMBE WA BODI WALIOTOA UDHURU

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Padre. Dkt. Charles Kitima | - | Mjumbe |
| 2. | Bi. Uphoo Swai | - | Mjumbe |

### WAGENI WAALIKWA

| | | | |
|---|---|---|---|
| ❖ | Bw. Baraka Palangyo | - | Mwakilishi wa PWC |
| ❖ | Bi. Neema Simika | - | Mwakilishi wa Benki Kuu ya Tanzania |
| ❖ | Bw. Grayson Anad | - | Mwakilishi wa Benki Kuu ya Tanzania |

## WANAHISA

| NA. | JINA | NAMBA YA CDS |
|---|---|---|
| 1 | ABEL BERA | 237272 |
| 2 | ABEL KUSIGA | 243361 |
| 3 | ABRAHAM A. MALEKO | 243368 |
| 4 | ADELAIDA ROGASIAN ASSEY | 237271 |
| 5 | ADRIAN J. MAKELELE | 243430 |
| 6 | ADRIANO G. MNIMBO | 243439 |
| 7 | AGATHA ELIAS MAYEMBA | 243449 |
| 8 | AGNES CHARLES KITWANGA | 235932 |
| 9 | AGNES FRANCIS MSOKA | 243460 |
| 10 | AGNES NJELDASEFO MARO MOSHA | 87941 |
| 11 | ALBANI PETER MWALO | 243523 |
| 12 | ALBART ALEXANDER | 243526 |
| 13 | ALBART HASSAN MILANZI | 140255 |
| 14 | ALEN EMIL RUBEN | 646814 |
| 15 | ALEX HENRY NYEREMBE | 248542 |
| 16 | ALEX MARKO | 249495 |
| 17 | ALEX SIMON NGAIZA | 236664 |
| 18 | ALEX STEPHANI KASILO | 237328 |
| 19 | ALFRED BENITO MILEMBE | 243610 |
| 20 | ALFRED CHAMA MATIKU | 243626 |
| 21 | ALINA BISTARI SHIRIMA | 243417 |
| 22 | ALPHONCE JOSEPH | 243708 |
| 23 | AMBROSE ROBERT LYIMO | 237168 |
| 24 | ANANIA K. WIGIRA | 243429 |
| 25 | ANASTAZIA D. MASHURANO | 243438 |
| 26 | ANDREA M. MGAYA | 235955 |
| 27 | ANDREW C. SHIRIMA | 103351 |
| 28 | ANNA ANTONY MVUNGI | 236057 |
| 29 | ANNA F. SHAO | 244379 |

| | | |
|---|---|---|
| 30 | ANNA SEIPH SHEMAGEMBE | 243552 |
| 31 | ANNA WANGAGI SWAI | 243559 |
| 32 | ANSILA JOHN | 236821 |
| 33 | ANTHONY OMARY DEWA | 243586 |
| 34 | ANUNTIATA MATHIAS KAWISHE | 246348 |
| 35 | ANZIGAR R. MAPINDA | 172059 |
| 36 | APOLINARY AMBROS MALLYA | 246352 |
| 37 | APOLINARY B. MWARABU | 236643 |
| 38 | ARCHIDIOCESE OF DAR ES SALAAM | 238712 |
| 39 | ARCHIDIOCESE OF DAR ES SALAAM | 238553 |
| 40 | ARCHIDIOCESE OF DAR ES SALAAM | 238724 |
| 41 | ARCHIDIOCESE OF DSM ITF JUMUIYA YA BIKRA MARIA WA LURDO | 238712 |
| 42 | ARCHIDIOCESE OF DSM JUMUIYA YA MT. MONICA | 238874 |
| 43 | ASUMTA V. IKOMKO | 243629 |
| 44 | AUDAX JOSEPHAT RUTA | 243647 |
| 45 | AUGUSTINE KISHULI | 243666 |
| 46 | AUGUSTINE PAULO MSETI | 243664 |
| 47 | AVELINA LUPINDA HEKORIRO | 243446 |
| 48 | BALBINA BALTAZARI SHAYO | 246423 |
| 49 | BALTHAZAR WARIOBA MWEIRO | 317424 |
| 50 | BARNABAS CHILALA | 243456 |
| 51 | BARTHOLOMEW J. KUNG'ALO | 215627 |
| 52 | BEATA NGADAKU EMILIUS | 243487 |
| 53 | BEATRICE BENN | 236048 |
| 54 | BEATUS COSMAS MWALONGO | 249713 |
| 55 | BELINDA SAKWARI | 237722 |
| 56 | BENEDICT JOACHIM MMASI | 212567 |
| 57 | BENEDICTO MAZIKU | 227647 |
| 58 | BENNET CHARLES MALEKELA | 153629 |
| 59 | BERNADETHA KATANDALU | 2498653 |
| 60 | BERTOLD THOMAS NJAWIKE | 243568 |

| | | |
|---|---|---|
| 61 | BERTWIN B. MANYAKU | 236888 |
| 62 | BETTY LEONARD MSHANA | 182609 |
| 63 | BIBIANA NGOWI | 243576 |
| 64 | BONECA GROUP LIMITED | 247280 |
| 65 | BONITUS DOMINIC MWALLENI | 243588 |
| 66 | CAMILLIAN FAMILY | 241123 |
| 67 | CARISTUS PHILIP ASSENGA | 244625 |
| 68 | CATHERINE C. MGAMA | 243635 |
| 69 | CATHERINE M. ANATHOLY | 244451 |
| 70 | CATHERINE MAJESA MWIDETE | 243632 |
| 71 | CELLINA D. MREFU | 237103 |
| 72 | CHARLES LUSANA | 236757 |
| 73 | CHARLES RUGALABAMU | 243714 |
| 74 | CHRISTA F. CHILALA | 243717 |
| 75 | CHRISTINA FABIAN KAPEMBE | 243728 |
| 76 | CLEMENT KIDALA | 236906 |
| 77 | CLEOPHACE ANGELUS NJOVU | 243772 |
| 78 | CLEVINA TIBAMANYA | 243778 |
| 79 | COMC SISTERS DIOCESE | 243124 |
| 80 | CONSOLATA ALBERT BEBWA | 324319 |
| 81 | COSTANTINE MALIGANYA | 249120 |
| 82 | COSTANTINO DANIEL MSIKE | 236896 |
| 83 | CUTHBERT KARUHANGA | 237039 |
| 84 | CYPIRIAN KRISPIN MDENDEMI | 130319 |
| 85 | CYRIL CHARLES MPOKAME | 236254 |
| 86 | DAMELA JOSEPH MWINUKA | 200441 |
| 87 | DANIEL JOHN KALLULYA | 2412181 |
| 88 | DANIEL M. UBALANJE | 236607 |
| 89 | DAUD JULIUS PANGILA | 243849 |
| 90 | DAYANA B. MGUMBA | 243865 |

| | | |
|---|---|---|
| 92 | DEOGRATIAS MODEST MTWALE | 236051 |
| 93 | DESIDERI J. MULAGALA | 244195 |
| 94 | DESIDERY KAKWEZI ATHANAS | 140802 |
| 95 | DEVINE PATRICK MATOLA | 234258 |
| 96 | DEVOTA PETER CHANWALI | 243691 |
| 97 | DIDAS SEIPH SHEMAGEMBE | 243706 |
| 98 | DIDAS SELESTIN MZIGAGAMBO | 243702 |
| 99 | DINA HAITA MBUBA | 235722 |
| 100 | DINA NGOTOLWA MASENGA | 243715 |
| 101 | DIOCESE OF MBINGA | 236237 |
| 102 | DIOCESE OF MOSHI | 240259 |
| 103 | DIOCESE OF MOSHI ITF JNNK MT. LUCIA KRISTO MFALME | 290259 |
| 104 | DIOCESE OF MTWARA | 240484 |
| 105 | DISMAS ISSA MLUNGAMO | 243716 |
| 106 | DISMASIA EDGA LYANGANI | 243720 |
| 107 | DOLORES DEOGRATIAS BARONGO | 242178 |
| 108 | DOMINIC  BEDA MASSAWE | 233815 |
| 109 | DONALD NKONGO CHACHA | 130040 |
| 110 | DONATUS PASKAL MLAY | 243730 |
| 111 | DORIS EDWARD NYATAHE | 238358 |
| 112 | DR JOHN B. TLEGRAY | 241343 |
| 113 | EDMUND ERNEST MUNISHI | 202118 |
| 114 | EDMUND MARKO | 249542 |
| 115 | EDWARD M. MWAIBAMBE | 250229 |
| 116 | EDWARDINA N. NGAIZA | 250230 |
| 117 | EDWIN PAUL MUNGA | 250234 |
| 118 | EDWINAAGNELLUS LUPEMBE | 244401 |
| 119 | ELIAS MMAZI | 246635 |
| 120 | ELIZABETH FRANK TOVO | 236054 |
| 121 | ELIZABETH IGNAS MOWA | 89497 |
| 122 | ELIZABETH MALONGO YINZA | 243735 |

| | | |
|---|---|---|
| 123 | ELIZABETH MBAGO | 243747 |
| 124 | ELIZABETH S. KABADI | 126336 |
| 125 | ELVIS GASPER KILAWE | 640891 |
| 126 | EMELDA CHARLES MWENDA | 236049 |
| 127 | EMELDA MEDARD KAVALO | 244434 |
| 128 | EMERENCIANA L. UTOU | 243760 |
| 129 | EMIL DAIMON ZAMBI | 165725 |
| 130 | EMMANUEL A. KULANGISIWA | 592126 |
| 131 | EMMANUEL CHILIPWELI | 243777 |
| 132 | EMMANUEL JULIUS BUKANGO | 248421 |
| 133 | EMMANUEL MAREKANI MTUI | 236622 |
| 134 | EMMANUEL SEIPH SHEMAGEMBE | 243788 |
| 135 | ENATA R. NONGA | 120134 |
| 136 | ENG. TRAUDA PIRMIN MUMBA | 237012 |
| 137 | ENOCK PH. KIKOTI | 243801 |
| 138 | ERICK AVELYN MARENGA | 244199 |
| 139 | ERICK BENEDICT SINDATUMA | 638995 |
| 140 | ERICK MWARABU | 250253 |
| 141 | ERICK RUBUVA | 243092 |
| 142 | ERICK W. MUSHI | 174809 |
| 143 | ESTER MWADUA MHANGA | 324574 |
| 144 | ESTERINA TARIMO | 246779 |
| 145 | ESTHER JULIUS BUKANGO | 248443 |
| 146 | ESTHER MTEMI | 250267 |
| 147 | EUTROPIA H. MARO | 250272 |
| 148 | EVANCE GASPAL LYIMO | 246838 |
| 149 | EVARIST ANTHONY MINANI | 250276 |
| 150 | EVE JOHN MKUNDI | 244420 |
| 151 | EWALD NEMES MREMA | 243875 |
| 152 | EXPEDITO DICKENS SIMMON | 237313 |
| 153 | EZEKIEL FELIX ISSAKA | 243886 |

| | | |
|---|---|---|
| 155 | FARAJA M. MASSAWA | 236931 |
| 156 | FAUSTA DAUDI CHILAMBO | 59516 |
| 157 | FAUSTER FAUSTINE KIWIA | 237028 |
| 158 | FAUSTUS GWIMO RUGONDA | 244207 |
| 159 | FEBROMA HILARY KAPINGA | 243912 |
| 160 | FEBRONIA I. SHEE | 243913 |
| 161 | FELISTER MPEMBA | 243916 |
| 162 | FIDELIS MARWA | 236756 |
| 163 | FLORA FILEMON MBINGA | 243937 |
| 164 | FLORENS IKIMOLO ISAKA | 243959 |
| 165 | FLORIAN D. MUTASIGWA | 249339 |
| 166 | FORTUNATA PATRICK CHAGU | 152878 |
| 167 | FR. ALEXUS C. MUTASIGWA | 237368 |
| 168 | FR.NIXON MBILLA | 234562 |
| 169 | FRANCIS BENEDICT SANGA | 248913 |
| 170 | GENEROSA JOSEPH RUTAIHWA | 252584 |
| 171 | GEOFREY PRINCE CALISTUS | 234566 |
| 172 | GEORGE TARIMO | 246917 |
| 173 | GERALD SAYI | 248036 |
| 174 | GERMANA G. MASUNGA ITF BRENDA | 236810 |
| 175 | GERVAS RAZARO MBILINYI | 243899 |
| 176 | GESMIRA SHAMGWA | 236689 |
| 177 | GETRUDE C. NGUBIAGAI | 236106 |
| 178 | GETRUDE J. TARIMO | 237315 |
| 179 | GIBSON KILALA | 625801 |
| 180 | GODFREY FOKAS MROSSO | 243838 |
| 181 | GODFREY MANDONDA KIBANDA | 59516 |
| 182 | GODFRIDA TESHA | 236981 |
| 183 | GODLIVER M. RWEYEMAMU | 237953 |
| 184 | GODWIN THOBIAS MWITA | 236628 |

| | | |
|---|---|---|
| 185 | GRACE BEDA | 237558 |
| 186 | GRACE DAVID MUSHI | 246968 |
| 187 | HAPINESS WADADI MSUMI | 235646 |
| 188 | HAPPY S. MREMA | 236633 |
| 189 | HELLEN MWANYIKA | 241305 |
| 190 | HENRY JOSEPH MBOYA | 140878 |
| 191 | HERMENIGIRDA MADILI | 250190 |
| 192 | IBRAHIM KASSALA NGETA | 24147 |
| 193 | IGNACE PETER MOWO | 243927 |
| 194 | IMACULATA D. MUTASHAIRWA | 139825 |
| 195 | IMAKULATA  CHAFUMBWE | 248938 |
| 196 | IMANI MUHINGO | 121217 |
| 197 | IRMINA MBULA MILLANZI | 250280 |
| 198 | JACKSON S. MTOKA | 243998 |
| 199 | JAMES KIWALI MALYA | 246956 |
| 200 | JANE JAPHET MALLYA | 244038 |
| 201 | JANE N. MUNISHI | 244437 |
| 202 | JANEMARY FAUSTINE RITAHOLE | 244045 |
| 203 | JANUARY MARIA NSHIMBA | 244075 |
| 204 | JASTAS SAUDI MKORONGO | 250818 |
| 205 | JEREMIA KADUMBA | 244097 |
| 206 | JERRY  MWASA | 248746 |
| 207 | JESCA JOEL | 244115 |
| 208 | JNN MT PADRE PIO | 238704 |
| 209 | JOACHIM PAUL MMASI | 244124 |
| 210 | JOAN CHAMUNGU MSUYA | 236959 |
| 211 | JOAN J. KAVISHE | 236656 |
| 212 | JOHN J. KILUWA | 2452239 |
| 213 | JOHN JOSEPH MNYIKAS | 235616 |
| 214 | JOHN MDENDE BIZONGWA | 244171 |

| | | |
|---|---|---|
| 216 | JOHN RAPHAEL KIMATA | 244151 |
| 217 | JOHN SEIPH SHEMAGEMBE | 244152 |
| 218 | JONAS DONAJI MLAY | 244438 |
| 219 | JORAH MWITA | 243732 |
| 220 | JOSEPH JAMES KESSY | 92371 |
| 221 | JOSEPH JOHN MBOJE | 238753 |
| 222 | JOSEPH N. HAULE | 250287 |
| 223 | JOSEPH NESTORY BUDELELE | 325066 |
| 224 | JOSEPH PHILIP MSAMI | 72861 |
| 225 | JOSEPH S. MREMA | 216127 |
| 226 | JOSEPH YESAYA KASYAMU | 236892 |
| 227 | JOSEPHAT PATRICK MBILINYI | 110729 |
| 228 | JOSEPHINE G. MABUBI | 238667 |
| 229 | JOSEPHINE JOHN MAZOMPOLA | 250294 |
| 230 | JOSEPHINE K. MUHULA | 111546 |
| 231 | JOYCE NALWAMBWA KAYESI | 250307 |
| 232 | JUDITH R. MKOBA | 112685 |
| 233 | JUDITH WENSLAUS NGAIZA | 249827 |
| 234 | JULIANA CHARLES MADELEKE | 236711 |
| 235 | JULIANA J. SHEMAGHUMBU | 142332 |
| 236 | JULIANA JOSEPH ANDREA | 236123 |
| 237 | JULIUS MBAWARA | 244297 |
| 238 | JUMANNE SAIDI SELEMANI | 237790 |
| 239 | JUMUIYA MT. CECILIA -M- NDEGE | 238767 |
| 240 | JUMUIYA YA MT IGNAS-MAKANGARAWE | 239088 |
| 241 | JUSTIN MARTIN MBATA | 250322 |
| 242 | KANDA YA FAMILIA TAKATIFU | 238667 |
| 243 | KARSTO ALFRED | 250334 |
| 244 | KELTRON MAHOO | 46683 |
| 245 | KOLETA MWALUGENGE | 250347 |
| 246 | KUMBUKA ENEA MANUZA | 236995 |

| | | |
|---|---|---|
| 247 | KWAYA FAMILIA TAKATIFU BUGURUNI | 238640 |
| 248 | KWAYA YA UPENDO | 236833 |
| 249 | LAMBERIHA MAHAI | 236913 |
| 250 | LAURENT MVUNGI | 249212 |
| 251 | LAWRENTIA M. MAYOLI | 236677 |
| 252 | LEOCADIA RWETI MKOJI | 236980 |
| 253 | LEONARDINA I. MAPUNDA | 250359 |
| 254 | LETICIA KWESA | 237032 |
| 255 | LETICIA M. CHAMBILA | 236062 |
| 256 | LEVINA MICHAEL MOMBURI | 236933 |
| 257 | LIDWIN LUVANDA | 250364 |
| 258 | LIGHTNESS CASTOR MBUTA | 250365 |
| 259 | LOUIZA STANLEY KESSY | 250375 |
| 260 | LUCAS A. BAYO | 250377 |
| 261 | LUCAS A. MAGALI | 236767 |
| 262 | LUCIANA ADRIAN MADUGA | 236683 |
| 263 | LUCY GEORGE MAYAO | 236835 |
| 264 | LUMINAT STANLEY KESSY | 250382 |
| 265 | LUTIGARDA LUCAS RWEZAULA | 235731 |
| 266 | MACRINA ANGELIMI KALINGA | 236684 |
| 267 | MAENDELEO GROUP | 241151 |
| 268 | MAJELINA MUSHUMBUJI | 244180 |
| 269 | MARCELLAR MARTIN KOMBA | 244188 |
| 270 | MARCELLINO XAVIER KAYOMBO | 228094 |
| 271 | MARIA FELIX SILAYO | 247236 |
| 272 | MARIA PETER DIMOSSO | 244435 |
| 273 | MARIANA NDONJEKWA | 244241 |
| 274 | MARKO JUSTINE MWENDA | 244255 |
| 275 | MARTIN KIMATH | 12211960 |
| 276 | MARTIN RAFAEL SIWINGA | 164635 |
| 277 | MARTINA I. MAKENI | 244280 |

| | | |
|---|---|---|
| 278 | MARY ELIAS KULIGWA | 244292 |
| 279 | MARY KILATU TEMBA | 236059 |
| 280 | MARY VICTORIA URASSA | 244947 |
| 281 | MATAUA HUGO SHIRIMA | 236687 |
| 282 | MATHIAS CYPIRIAN MKULA | 244337 |
| 283 | MATHIAS JAMES | 227207 |
| 284 | MATHIAS L. LAURENT | 244342 |
| 285 | MATHIAS MUJUAMUNGU | 244333 |
| 286 | MATLIDA STANSLAUS KALOKOLA | 244169 |
| 287 | MAY MUNGILWA | 236694 |
| 288 | MBOJE RICHARD | 245021 |
| 289 | MECTIDIS C. SHONGA | 245120 |
| 290 | MEDARD JOHN KAVALO | 236978 |
| 291 | MELANIA C. MAGOTI | 244212 |
| 292 | MELKIADES F. MSIMBE | 247204 |
| 293 | METIDIS CONRAD VYANEY UNGA | 236890 |
| 294 | MICHAEL URIO | 244294 |
| 295 | MICHAEL YEREMIAH LUVAGA | 325446 |
| 296 | MODEST PETER MWALO | 244372 |
| 297 | MOHAMED SALIM MHARIZ | 235910 |
| 298 | MOSHI UNITED GROUP | 237285 |
| 299 | MSHOBOZI P. ABDOR | 100356 |
| 300 | NAZARIUS PAUL CHONYA | 244473 |
| 301 | NEEMA M. NUNGU | 244479 |
| 302 | NESSY ELIAS KYEJO | 236866 |
| 303 | NICODEMAS J. KANJE | 237694 |
| 304 | NICODEMUS JOSEPH KISHEO | 236956 |
| 305 | OCTAVIAN MSOFU | 237709 |
| 306 | ODILIA KILIAN KIWASILA | 233444 |
| 307 | OFORO ANDREA ERASMO | 245688 |
| 308 | OLIVER A. KULANGISIWA | 236706 |

| | | |
|---|---|---|
| 309 | OSCAR MECK MANSHA | 223016 |
| 310 | OSCAR PIUS MSANGIRA | 249716 |
| 311 | OTHMAN MAALIM ZARAL | 235909 |
| 312 | PANCRAS SAMWEL TAIRO | 244407 |
| 313 | PASCHAL MALIFEDHA KANYALA | 237010 |
| 314 | PASTORY MATEI MISANYA | 236907 |
| 315 | PAUL KALINJUMA DAUDI | 242874 |
| 316 | PAUL SALUMU SHEMETA | 244522 |
| 317 | PAULINA MANULU | 134947 |
| 318 | PELAD J. TARIMO | 186249 |
| 319 | PELAGIA KAWAMALA CHARLES | 140125 |
| 320 | PERPETUA E. ISHABAKAKI | 244547 |
| 321 | PETER KESSY | 236152 |
| 322 | PETER KIPANGULU | 249128 |
| 323 | PETER MWITA NYANOKWE | 163818 |
| 324 | PHILEMON AMBROSE MUSHI | 244582 |
| 325 | PHILIP LAWRENCE MJEMA | 76901 |
| 326 | PIUS GABRIEL SIRIWA | 247508 |
| 327 | PIUS KITOSI | 244611 |
| 328 | PRAXEDY VINCENT CHACKY | 236676 |
| 329 | PRIMITIVA PATRICK KAMUGISHA | 220431 |
| 330 | PRISCILLA RASHIDI | 244604 |
| 331 | PROGENETHA K. IBRECK | 319688 |
| 332 | PULICERIA EMILY MASSAWE | 236717 |
| 333 | RASHID A. KUPYASA | 236972 |
| 334 | RAY ELIAKIMU KIMBITORY | 244670 |
| 335 | RAYNALDA FIDEUS NGOMBARE | 235696 |
| 336 | REGINA AUGUSTINO HINGA | 59516 |
| 337 | REGINA JOEL KABALIBAL | 24405 |
| 338 | REGINA KAGEMULO MHINA | 236951 |
| 339 | RENATUS R. MWAKIMBWALA | 250735 |

| | | |
|---|---|---|
| 340 | RESPICIOUS S. MULISA | 242861 |
| 341 | REUBEN PETER MMAJE | 15916 |
| 342 | REVOCATUS RUSTICUS MSHEMA | 244710 |
| 343 | RICHARD KABYEMELA | 118108 |
| 344 | RICHARD M. KAYOMBO | 244589 |
| 345 | ROHM MILAN DIVECHA | 235666 |
| 346 | ROMANIA V. LASWAY | 247541 |
| 347 | ROSADA SHAO | 250423 |
| 348 | ROSE FRANCIS MAIGE | 244366 |
| 349 | ROSE MBUTA | 250435 |
| 350 | RUCU | 241196 |
| 351 | RUDOLF ATILIO MKEMWA | 237232 |
| 352 | RUSALIA DIDAS | 52789 |
| 353 | RUSTUS | 238380 |
| 354 | SABAS MROSSO | 216526 |
| 355 | SABINA MWENDA LUTUO | 339728 |
| 356 | SABINA ARBETI MWAHELYA | 238382 |
| 357 | SABINA MOSHY | 235936 |
| 358 | SAHIMBA J. MSEMWA | 325822 |
| 359 | SALAME C. MAKAMBI | 236724 |
| 360 | SALUSTIAN THOBIAS NKOLA | 236793 |
| 361 | SALVATORY JOHAKIM | 98153 |
| 362 | SARAFINA BENARD SAYI | 248075 |
| 363 | SARAHS S. MTILEMA | 250546 |
| 364 | SCHOLA A. MASAWE | 236947 |
| 365 | SCHOLASTICA JOHN MTIRUKA | 245676 |
| 366 | SEBASTIAN SIMBA LUHEJA | 244417 |
| 367 | SECHELELA HOKORORO | 237017 |
| 368 | SELINA MLINGI | 236842 |
| 369 | SH. BIKRA MARIA MSAADA KRISTO | 248 |
| 370 | SIMON NDETMBEA SWATI | 237311 |

| | | |
|---|---|---|
| 371 | SIMON P. MRINA | 244661 |
| 372 | SOPHIA GALLE MBWILLE | 235625 |
| 373 | SOPHIA S. MZENA | 235711 |
| 374 | SPECIOZA M. KAVALO | 237008 |
| 375 | ST AUGUSTINE UNIVERSITY OF TANZANIA | 241539 |
| 376 | ST CHARLES LWANGA SEGEREA SENIOR MISSIONARY | 241173 |
| 377 | ST GEMALA GAIGAN SISTERS | 241172 |
| 378 | ST JOHN BOSCO PARISH KIBAHA | 237737 |
| 379 | STANSLAUS WILLIAM MIZAMBWA | 244724 |
| 380 | STANSLAUS E. MZENA | 232274 |
| 381 | STELLA CHARLES MIHAMBO | 237129 |
| 382 | STELLA PANTALEO BUNDALA | 236728 |
| 383 | SUBIRA ROGATH KIMARIO | 244736 |
| 384 | SUSANA RHOBI MUHAGACHI | 244361 |
| 385 | TANZANIA EPISCOPOL CONFERENCE (TEC) | 241259 |
| 386 | TAUSI ROBATI KWIMBA | 236388 |
| 387 | TEDDY ANDREW SALUMU | 244749 |
| 388 | TEOTIM RICHARD MMANDA | 9694108 |
| 389 | THADEO PIUS KABUNDUGULU | 236732 |
| 390 | THECLA INNOCENT MALINDI | 244783 |
| 391 | THEODASIA THOMAS CHUWA | 244819 |
| 392 | THEODORA SABINI MAKAWISHE | 247764 |
| 393 | THEOPISTA STEPHEN TARIMO | 247773 |
| 394 | THERESIA EPAFRASI KESSY | 247802 |
| 395 | THERESIA NJENDELA MAPUNDA | 144487 |
| 396 | THERESIA ZAWADI NKUNJA | 244896 |
| 397 | THOMAS J. NGWALA | 6236865 |
| 398 | THOMAS JULIUS MWARA | 236865 |
| 399 | UFUMWA SACCOS | 241569 |
| 400 | UPENDO KAYOMBO | 244972 |

| | | |
|---|---|---|
| 401 | USAMBARA SISTERS KURASINI | 241289 |
| 402 | USHIRIKA WA NGONYAMA | 241297 |
| 403 | UTOTO MT MSIMBAZI | 238657 |
| 404 | VALENCE ADRIAN KATUMA | 236741 |
| 405 | VENERIUS STANSLAUS MUBA | 236923 |
| 406 | VERDIANA MASSINDE MARGAI | 245044 |
| 407 | VEREDIANA VALERIANI MUNISHI | 250442 |
| 408 | VERONICA GAETANO KIBIKI | 245062 |
| 409 | VERONICA LUCAS | 245083 |
| 410 | VERONICA ROCHUS KANWERA | 236986 |
| 411 | VERONICA T KIIZA | 245092 |
| 412 | VIANEY LUNGA | 236890 |
| 413 | VICTOR FELICIAN MUTTA | 488149 |
| 414 | VICTORIA A. GANAI | 237294 |
| 415 | VICTORIA CLEMENT LIKWEMBA | 215141 |
| 416 | VICTORIA ERNEST LUKUMBA | 132420 |
| 417 | VINCENTE MPUPUA | 245180 |
| 418 | VIRGINIA VUMILIA | 243050 |
| 419 | WAKILI S. ALAWI | 245230 |
| 420 | WENSE L. ULIMALI | 245240 |
| 421 | WILLIAM KALAYE | 7633 |
| 422 | WINFRIDA M. MNONJELA | 237009 |
| 423 | WINFRIDA PATRICK KAMUGISHA | 235703 |
| 424 | WOLFGANG E. SALIA | 522274 |
| 425 | YAVAN SHEDRACK FOYA | 245623 |
| 426 | YOHANA MBATIZAJI KIGILAGILA | 238970 |
| 427 | YOLATHA BAZIL TARIMO | 236944 |
| 428 | ZACHARIA ANDREA MAHANJILE | 237210 |

## 1.0 KUFUNGULIWA KWA MKUTANO

Mwenyekiti alifungua rasmi Mkutano saa 03:40 asubuhi.

## 2.0 KUPITISHWA KWA AJENDA

Ajenda zifuatayo zilipitishwa:

1. Kufungua Mkutano;
2. Kupitishwa kwa ajenda;
3. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Tano wa Mwaka uliofanyika 27 Julai, 2024;
4. Kupokea na kujadili mambo yanayotokana na Mkutano Mkuu wa Kumi na Tano wa Mwaka uliofanyika tarehe 27 Julai 2024;
5. Kupokea, kujadili na kuidhinisha taarifa ya Wakurugenzi kwa mwaka ulioishia 31 Desemba 2024;
6. Kupokea, kujadili na kuidhinisha taarifa za fedha za Benki na taarifa ya mkaguzi wa nje kwa mwaka ulioishia 31 Desemba 2024;
7. Pendekezo la kutoa Gawio la Mwaka 2024;
8. Uteuzi wa Mkaguzi wa Nje wa Hesabu za Benki;
9. Uchaguzi wa Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi;
11. Kupendekeza Tarehe ya Mkutano Mkuu wa Mwaka ujao;
12. Mengineyo; na
13. Kufunga Mkutano

## 3.0 UTHIBITISHO WA DONDOO ZA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA KUMI NA TANO ULIOFANYIKA TAREHE 27 JULAI, 2024.

3.1 Wanahisa walithibitisha Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Tano wa Mwaka uliofanyika tarehe 27 Julai 2024 baada ya kufanya marekebisho madogo madogo ya kiuandishi.

## 4.0 KUPOKEA NA KUJADILI YATOKANAYO NA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA KUMI NA TANO ULIOFANYIKA TAREHE 27 JULAI 2024.

4.1 ILIRIPOTIWA kwamba maelekezo ya wanahisa kuhusu kuboresha taarifa katika daftari la wanahisa kwa kuhakikisha taarifa za majina, mawasiliano na malipo ya gawio zinakuwa sahihi na zinahuishwa yalitekelezwa, na yanaendelea kuwa sehemu ya ajenda ya benki. Benki ilianzisha dawati maalum la kushughulikia masuala ya wanahisa, ikiwemo kuhuisha taarifa za wanahisa na malipo ya gawio. Aidha, benki imekuwa ikitumia fursa ya uwepo wa wanahisa katika Mikutano Mikuu ya Mwaka

kuthibitisha na kuhuisha taarifa zao. Kufuatia tangazo la gawio lililotolewa tarehe 19 Mei 2025, benki pia ilianza jitihada kupitia matawi yake kuwafikia wanahisa na kuhuisha taarifa zao ipasavyo.

4.2. ILIRIPOTIWA kwamba maelekezo ya kuboresha utendaji wa benki na kutekeleza miradi iliyopangwa ili kuiwezesha benki kuwa katika nafasi ya kulipa gawio kwa mwaka uliofuata yalitekelezwa. Benki iliboresha kwa kiasi kikubwa utendaji wake katika viashiria vyote muhimu kwa mwaka wa fedha 2024 na kutokana na mafanikio hayo, ikaweza kulipa gawio kuanzia tarehe 15 Agosti 2025 baada ya Mkutano Mkuu wa Mwaka.

4.3 ILIRIPOTIWA kwamba maelekezo ya kuzingatia viwango vya udhibiti vya Benki Kuu ya Tanzania (BOT), hususan uwiano wa mikopo chechefu (NPL) na uwiano wa gharama dhidi ya mapato (CIR), ili kuiwezesha benki kulipa gawio katika Mwaka uliofuata, yalitekelezwa. Kulikuwa na mafanikio makubwa ambapo benki iliboresha uwiano wa gharama dhidi ya mapato kutoka 62% hadi 57%, kiwango ambacho kiko karibu na kiwango elekezi cha udhibiti cha 55%. Aidha, uwiano wa mikopo chechefu (NPL) uliboreshwa kutoka 8% hadi 3.8%, kiwango ambacho kiko ndani ya kiwango elekezi cha 5%. Kutokana na matokeo hayo yaliyoboreshwa Benki Kuu ya Tanzania iliidhinisha malipo ya gawio kwa mwaka 2024.

4.4 ILIRIPOTIWA kwamba maelekezo ya kutafuta fursa za biashara katika maeneo mbalimbali ikiwemo Ifakara na Njombe, pamoja na kuchunguza fursa nyingine za utoaji huduma na bidhaa kwa wanafunzi, vijana na sekta isiyo rasmi, yalitekelezwa na yanaendelea kuwa sehemu ya mwelekeo wa benki. Benki iliimarisha mkakati wake wa usajili na usimamizi wa biashara kwa kuendelea kuzingatia soko lake la kimkakati, ambalo ni Kanisa na taasisi zake. Benki ilizindua suluhisho mbalimbali kwa makundi ya kimkakati ya wateja, ikiwemo parokia na mnyororo wake wa thamani, hospitali, taasisi za elimu ya juu na shule. Aidha, benki iliboreshwa bidhaa ya Akaunti ya Wanafunzi kwa kuongeza huduma na vivutio vinavyorahisisha matumizi, ikiwa ni sehemu ya mkakati mpana wa kujenga utamaduni wa matumizi ya huduma za benki kwa vijana na kuimarisha ubora wa huduma za Benki kwa kizazi hicho. Benki pia ilipanua huduma zake za mikopo kwa kuanzisha bidhaa ya "Mikopo Midogo" inayolenga wafanyabiashara binafsi wanaokua kutoka kundi la mikopo ya vikundi ("Solidarity Group Loans").

4.5 ILIRIPOTIWA kwamba maelekezo ya kuhamasisha Kanisa na taasisi zake kutumia mifumo ya benki katika kufanya miamala mbalimbali yalitekelezwa na yanaendelea kufuatiliwa. Benki iliandaa huduma na suluhisho mbalimbali kukidhi mahitaji ya makundi tofauti ya wateja ndani ya mwavuli wa Kanisa. Sambamba na hilo, benki iliimarisha uwezo wake wa utoaji huduma kupitia mifumo ya kidijitali kama mawakala wa Mkombozi, huduma za kibenki kwa njia ya mtandao na huduma za kibenki kwa njia ya simu. Malengo ya kimkakati ya ukuaji na faida ya benki yamejengwa katika soko la Kanisa kama soko maalum, hivyo utekelezaji wa mikakati utaendelea kuzingatia eneo hilo muhimu.

4.6 ILIRIPOTIWA kwamba maelekezo ya kuhakikisha nyaraka za Mkutano Mkuu wa Mwaka zinaandaliwa kwa idadi ya kutosha na kusambazwa kwa wanahisa wote kwa wakati ili kuwezesha ushiriki mzuri katika mkutano yalitekelezwa. Benki ilihakikisha kuwa nyaraka za Mkutano Mkuu wa 16 ziliandaliwa kwa kiwango kilichokidhi wanahisa wote waliohudhuria mkutano huo. Aidha, nyaraka hizo zilisambazwa kwa wanahisa wote mwezi mmoja kabla ya mkutano kufanyika.

4.7 ILIRIPOTIWA kwamba maelekezo ya kushughulikia changamoto zilizobainika katika mfumo wa huduma za kibenki kwa njia ya mtandao, huduma za uwakala wa benki, pamoja na kuboresha ufanisi wa utoaji huduma katika matawi yote ya benki, yalitekelezwa na yanaendelea kuwa sehemu ya vipaumbele vya utekelezaji. Benki ilifanya maboresho makubwa katika mifumo yake ya kidijitali, ikiwemo huduma za kibenki kwa njia ya mtandao, huduma za benki kwa wakala na huduma za benki kwa njia ya simu. Maboresho hayo yalienda sambamba na uboreshaji wa mfumo mkuu wa benki ambao umechangia kuimarika kwa uthabiti na utendaji wa mifumo hiyo. Kutokana na hatua hizo, kumekuwa na ongezeko kubwa la ufanisi katika utoaji huduma kupitia matawi ya benki pamoja na majukwaa yake ya kidijitali.

## 5.0 KUPOKEA, KUJADILI NA KUIDHINISHA TAARIFA YA BODI YA WAKURUGENZI KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DISEMBA 2024

5.1. ILIRIPOTIWA kuwa Benki iliendelea kutoa huduma za kibenki na kifedha kwa mujibu wa Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na kwamba hakukuwa na mabadiliko yoyote katika shughuli kuu za Benki kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2024.

5.2. ILIRIPOTIWA kuwa jumla ya hisa 23,555,002 zenye thamani ya shiling 22,820,069,500 zilikua zimelipiwa kikamilifu.

5.3. ILIRIPOTIWA kuwa jumla ya Wakurugenzi wanane (8), akiwemo Mkurugenzi Mtendaji, walihudumu katika Benki katika kipindi hicho na hakuna Mkurugenzi aliyekuwa anamiliki zaidi ya asilimia 0.1 ya mtaji wote wa hisa uliotolewa na Benki.

5.4. ILIRIPOTIWA kuwa Bodi ya Wakurugenzi iliendelea kuhakikisha kuwa taratibu na kanuni zote za kibenki zinafuatwa kwa mujibu wa mfumo wa uendeshaji wa Benki. Aidha, shughuli za kila siku za kibenki ziliendelea kusimamiwa na Mkurugenzi Mtendaji akisaidiwa na Timu ya Menejimenti.

5.5. ILIRIPOTIWA kuwa Benki ilipata Faida Kabla ya Kodi (PBT) ya Shilingi milioni 11,493 kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2024 ikilinganishwa na Shilingi milioni 8,572 mwaka 2023. Viashiria vingine vya utendaji vilikuwa kama ifuatavyo:-

5.5.1. Mapato Halisi ya Uendeshaji yaliongezeka hadi Shilingi milioni 29,216 kutoka Shilingi milioni 25,226 mwaka 2023. Ukuaji huo ulitokana na ongezeko la Shilingi milioni 4,631 (26%) katika mapato ya riba, likichangiwa na uimara wa mizania ya Benki pamoja na kupungua kwa gharama za riba kwa 5% (Shilingi milioni 361) kupitia usimamizi mzuri wa muundo wa amana.

5.5.2. Amana za wateja ziliongezeka hadi Shilingi milioni 217,491 kutoka Shilingi milioni 207,397 mwaka 2023, sawa na ukuaji wa 5%, uliotokana na mikakati ya uhamasishaji wa amana pamoja na maboresho ya miundombinu ya kibenki, ikiwemo njia za kidijitali.

5.5.3. Jumla ya mali za Benki ziliongezeka hadi Shilingi milioni 282,380 kutoka Shilingi milioni 255,789 mwaka 2023, hasa kutokana na ongezeko la Shilingi milioni 28,304 katika mikopo kwa wateja na benki nyingine.

5.5.4. Jumla ya gharama za uendeshaji ziliongezeka hadi Shilingi milioni 17,723 ikilinganishwa na Shilingi milioni 16,654 mwaka 2023. Ongezeko hilo la 6% lilitokana na upanuzi wa biashara na kuongezeka kwa shughuli za uendeshaji.

5.5.5. Mikopo iliongezeka hadi Shilingi milioni 162,565 kutoka Shilingi milioni 134,261 mwaka 2023, sawa na ukuaji wa 21%. Ukuaji huo ulitokana na kuboreshwa kwa mifumo ya utoaji mikopo pamoja na kuimarika kwa kiwango cha mtaji wa Benki.

5.5.6. Ubora wa kitabu cha mikopo uliendelea kuwa mzuri ambapo uwiano wa mikopo chechefu (NPL) ulifikia 3.8% mwaka 2024.

5.6. ILIRIPOTIWA kuwa Bodi ya Wakurugenzi ilifanya tathmini ya uwezo wa Benki kuendelea kujiendesha (going concern) na matokeo yalionyesha kuwa Benki itaendelea kuendesha shughuli zake kwa kipindi kirefu kijacho.

5.7. ILIRIPOTIWA kuwa Bodi ya Wakurugenzi ilipendekeza malipo ya gawio kwa wanahisa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2024.

5.8. ILIRIPOTIWA kuwa Benki ilikuwa na wafanyakazi wa kutosha wenye uzoefu wa kutekeleza shughuli zake na kufanikisha mpango wa biashara wa Benki.

5.9. ILIRIPOTIWA kuwa Benki haikutoa msaada kwa chama chochote cha siasa na iliendelea kuwa na mahusiano mazuri na wadau wote, ikiwemo kamati za usimamizi wa benki.

5.10. ILIRIPOTIWA kuwa Benki ilikamilisha utekelezaji wa mfumo mpya wa kibenki wa msingi (RUBIKON) na kuhamisha shughuli zote za huduma za kibenki kwenye mfumo huo.

5.11. ILIRIPOTIWA kuwa Benki ilikamilisha mradi wa mfumo wa Usimamizi wa Shule na kuanza kuusambaza mashuleni, ikiwa imelenga kuuuza mfumo huo kwa shule 200 ifikapo mwaka 2026.

5.12. ILIRIPOTIWA kuwa huduma za kidijitali za Benki ziliendelea kukua kwa kasi. Huduma za "Mkombozi Wakala", "Sadaka Digital", huduma za kibenki kwa njia ya mtandao na huduma za kibenki kwa njia ya simu ziliongeza matumizi na kufikia wateja wengi zaidi.

5.13. ILIRIPOTIWA kuwa Benki ilitekeleza mradi wa ushirikiano wa matumizi ya mashine za kutolea hela yaani ATM kati yake na NMB Bank Plc kupitia Umoja Switch inayowezesha wateja wa benki kupata huduma kupitia mtandao wa ATM za NMB Bank Plc.

5.14. ILIRIPOTIWA kuwa Benki ilitekeleza Mfumo wa Usimamizi wa Fedha katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino Tanzania (SAUT) kwa ajili ya ukusanyaji ada na ilikuwa katika hatua za kuusambaza mfumo huo katika taasisi nyingine za elimu ya juu ndani ya soko la kimkakati la Benki.

5.15. ILIRIPOTIWA kuwa Benki ilikamilisha Mfumo wa Usimamizi wa Hospitali na kuanza hatua za usajili katika Hospitali ya Bugando, huku ikipanga kuusambaza katika vituo vingine vya afya ndani ya soko lake maalum.

5.16. ILIRIPOTIWA kuwa Benki ilianza maandalizi ya kupanua mtandao wa matawi yake kwa lengo la kufungua matawi matatu mapya mwaka 2025.

5.17. ILIRIPOTIWA kuwa jitihada za Benki katika kuimarisha biashara na kukuza shughuli zake ziliendelea kuzaa matunda kupitia ongezeko la wateja, mapato, usimamizi bora wa gharama na usimamizi wa vihatarishi kwa ufanisi.

5.18. ILIRIPOTIWA kuwa wanahisa waliipongeza Benki kwa utendaji wake wa mwaka 2024 na kutoa maoni yafuatayo:-

5.18.1 Wanahisa waliuliza kama huduma za kibenki kwa njia ya simu zinahitaji salio la muda wa maongezi (airtime). Benki ilieleza kuwa huduma za kibenki kwa simu kwa njia ya USSD zinahitaji mteja awe na salio la maongezi (airtime) wakati huduma za kibenki kwa njia ya programu (application) zinahitaji huduma ya intaneti.

5.18.2 Wanahisa walibaini kuwa gharama za mafunzo kwa wafanyakazi zilikuwa chini ya bajeti na kuhoji kama wafanyakazi walipata mafunzo ya kutosha. Menejimenti ilieleza kuwa Benki ilitumia mfumo wa mafunzo unaojumuisha wakufunzi wa ndani na nje, mafunzo ya mtandaoni na mafunzo ya vikundi, hali iliyosaidia kupunguza gharama za utoaji wa mafunzo huku ubora ukiendelea kudumishwa.

5.18.3 Wanahisa waliuliza kama upanuzi wa matawi unategemea uwepo wa Jimbo la Kanisa. Benki ilieleza kuwa maamuzi ya kufungua matawi mapya huzingatia fursa za biashara, uwezo wa kuzalisha mapato na kurudisha uwekezaji, sambamba na kuzingatia viwango vya uwiano wa gharama dhidi ya mapato uliowekwa na Benki Kuu.

5.18.4 Wanahisa waliipongeza Benki kwa ushirikiano wake na benki ya NMB katika utoaji wa huduma za kibenki kwa njia ya mashine za kutolea pesa (ATM) na kuuliza kama Benki ina mpango wa kuanzisha bidhaa za uwekezaji wa hati fungani siku za usoni. Bodi ilieleza kuwa bidhaa ya hati fungani huongeza gharama zariba kwa taasisi hivyo Benki itaendelea kuhamasisha zaidi amana za gharama nafuu kupitia akaunti za akiba na akaunti za hundi (CASA).

5.18.5 Wanahisa walipendekeza kuanzishwa kwa bidhaa maalum kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo, vikundi maalumu na wanawake. Benki ilieleza kuwa tayari imeanzisha mikopo maalumu kuhudumia makundi tajwa hapo

juu kwa kutoa mikopo kwa wateja na wajasiriamali wadogo, vikundi na wanawake kwa ujumla.

5.18.6 Wanahisa walipendekeza kuwepo kwa viwango maalum vya riba na tozo za mikopo kwa wanahisa. Bodi ilieleza kuwa kanuni za Benki Kuu haziruhusu wanahisa kupewa masharti nafuu kuliko wateja wengine na hivyo wanahisa waendelee kutumia bidhaa na huduma za benki zinazotolewa kwa gharama na masharti nafuu sana.

5.18.7 Wanahisa walieleza wasiwasi wao kuhusu viwango vya tozo za miamala. Bodi ilipokea maoni hayo na kuahidi kufanya mapitio ya viwango vya tozo ili kuongeza ushindani na unafuu kwa wateja.

5.18.8 Wanahisa waliuliza kama wanaweza kununua hisa zaidi za Benki na Bodi ilieleza kuwa hisa za Benki zinaendelea kuuzwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam na kuwataka wanahisa kutumia madalali waliosajiliwa katika uuzaji na ununuzi wa hisa za benki.

5.18.9 Wanahisa walibaini kuwa Benki bado ina matawi machache katika baadhi ya maeneo na kushauri kuendelea kupanua huduma kwa kuongeza matawi na utoaji wa huduma kwa njia za kidijitali. Benki iliahidi kuendelea kuimarisha utoaji huduma kwa kufungua matawi zaidi, kupitia mawakala na mifumo ya kidijitali.

5.18.10 Wanahisa walishauri Benki kuongeza nguvu katika kutangaza bidhaa na huduma zake kupitia majukwaa ya Kanisa. Bodi ilieleza kuwa Benki inaendelea kutumia makanisa, parokia, vyombo vya habari vya Kanisa na mitandao ya kijamii kuongeza uelewa wa bidhaa na huduma zake.

5.18.11 Wanahisa walieleza kuwa Kanisa na taasisi zake zina fursa kubwa za biashara na kuitaka Benki kuongeza ushirikiano katika soko hilo maalum. Bodi ilikubaliana na ushauri huo na kuahidi kuongeza ushirikiano na taasisi za Kanisa.

5.18.12 Wanahisa walipendekeza mikutano mikuu ijayo ifanyike pia katika mikoa mingine nje ya Dar es Salaam ili kurahisisha ushiriki wa wanahisa kutoka mikoani. Bodi ilipokea ushauri huo kwa ajili ya utekelezaji kwa siku za baadaye.

6.0 ILIRIPOTIWA kuwa Wanahisa walitoa MAAGIZO yafuatayo kufuatia maoni yaliyotolewa hapo awali:

6.1 Kuanzisha mfumo katika ngazi ya matawi utakaowezesha wanahisa kusahisha na kurekebisha taarifa zao katika rejista ya wanahisa.

6.2 Kurahisisha na kuboresha mchakato wa kufungua akaunti ili kuongeza usajili wa wateja utakaoleta uhamasishaji na ongezeko la amana na uwekezaji.

6.3 Kutumia kikamilifu fursa zilizopo katika soko maalum la Benki, hususan shule, hospitali na vyuo vinavyohusiana na Kanisa, ili kukuza biashara na utendaji wa Benki.

6.4 Kukamilisha utekelezaji wa miradi yote iliyopangwa kwa mwaka 2025.

6.5 Kuendelea kufanya ziara kwa wateja katika parokia na maeneo yenye fursa za biashara kwa ajili ya uhamasishaji wa amana, ushirikiano na ufadhili wa miradi mbalimbali.

6.6 Kufanya mapitio ya viwango vya tozo za Benki kwa kuzingatia maoni ya wanahisa kuhusu kupungiza gharama za huduma.

6.7 Kuendelea kuhamasisha Kanisa na taasisi zake kutumia Benki na mifumo yake katika kufanya miamala mbalimbali.

6.8 Kutumia majukwaa ya Kanisa kutangaza bidhaa na huduma za Benki ili kuongeza mwonekano na mwitikio wake sokoni.

6.9 Kuimarisha uwepo wa Benki katika mikoa mbalimbali kupitia ufunguzi wa matawi na vituo vya huduma kwa kuzingatia uwezo wa mtaji na mkakati wa ukuaji.

6.10 Kuzingatia mzunguko wa maeneo ya kufanyia mkutano mkuu wa wanahisa katika mikoa muhimu kama Mwanza, Dodoma na Arusha ili kurahisisha ushiriki wa wanahisa kutoka mikoani.

6.11 ILIRIPOTIWA kuwa wanahisa walipokea, walijadili na kuidhinisha Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi.

## 7.0. KUPOKEA, KUJADILI NA KUIDHINISHA TAARIFA ZA FEDHA ZA BENKI PAMOJA NA TAARIFA YA MKAGUZI WA NJE KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DISEMBA 2024.

7.1 ILIRIPOTIWA kwamba Mkaguzi wa Nje wa Benki kwa mwaka 2024 alikuwa ni Kampuni ya PricewaterhouseCoopers (PWC).

7.2 ILIRIPOTIWA kuwa kufikia tarehe 31 Desemba 2024, Wakaguzi wa Nje walikuwa wamekagua taarifa ya hali ya fedha ya Benki, mapato, taarifa ya mabadiliko katika mtaji usio na riba, taarifa ya mtiririko wa fedha ya mwaka, muhtasari wa sera za uhasibu pamoja na maelekezo mengine ya kifedha ya mwaka uliopita.

7.3 ILIRIPOTIWA kuwa kwa mujibu wa maoni ya Wakaguzi wa Nje, taarifa za fedha zilizokaguliwa zilionesha kwa usahihi hali ya kifedha ya Benki kufikia tarehe 31 Desemba 2024 kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Utoaji Taarifa za Fedha (IFRSs), matakwa ya Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002 pamoja na Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006.

7.4 ILIRIPOTIWA kuwa Wakaguzi wa Nje walifanya ukaguzi wao kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Hesabu (ISAs).

7.5 ILIRIPOTIWA kuwa Wakaguzi wa Nje walipata taarifa zote na maelezo ambayo, kwa kadri ya ufahamu na imani yao, yalikuwa muhimu kwa madhumuni ya ukaguzi huo.

7.6 ILIRIPOTIWA kuwa kwa maoni ya Wakaguzi wa Nje, Benki ilihifadhi vitabu sahihi vya hesabu; Taarifa ya Wakurugenzi ilikuwa inaendana na taarifa za fedha; taarifa zinazotakiwa kisheria kuhusu malipo ya Wakurugenzi na miamala yao na Benki zilikuwa zimewekwa wazi; na taarifa ya hali ya fedha pamoja na taarifa ya faida au hasara na mapato mengine jumuishi zilikuwa zinaendana na vitabu vya hesabu vya Benki.

7.7 ILIRIPOTIWA kuwa kwa maoni ya Wakaguzi wa Nje, viwango vya utoshelevu wa mtaji wa Benki vilivyowasilishwa vilikokotolewa kwa mujibu wa Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, Kanuni za Utoshelevu wa Mtaji za mwaka 2014 pamoja na maelekezo husika ya Benki Kuu ya Tanzania.

7.8 ILIRIPOTIWA kuwa wanahisa walipokea, walijadili na kuidhinisha taarifa za fedha za Benki pamoja na taarifa ya Mkaguzi wa Nje kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2024.

## 8.0 PENDEKEZO LA KUTOA GAWIO LA FAIDA KWA MWAKA 2024

8.1 ILIRIPOTIWA kwamba katika Mkutano Maalum wa 120 wa Bodi ya Wakurugenzi uliofanyika tarehe 26 Machi 2025, Bodi ya Wakurugenzi ilipokea na kuidhinisha Taarifa za Fedha za Benki kwa mwaka 2024.

8.2 ILIRIPOTIWA kwamba kwa mujibu wa Ibara ya 109 na Ibara ya 140 za Mkataba na Kanuni za Uanzishwaji wa Benki, Bodi ya Wakurugenzi ilipendekeza malipo ya gawio la Shilingi 92.40 kwa kila hisa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2024, kwa wanahisa wote waliokuwemo kwenye rejesta ya wanahisa kufikia tarehe 3 Julai 2025, ambapo rejesta itafungwa na malipo kufanyika kuanzia tarehe 15 Agosti 2025.

8.3 ILIRIPOTIWA kwamba Wanahisa waliombwa kupokea, kujadili na kuidhinisha pendekezo la Bodi ya Wakurugenzi la kulipa gawio la Shilingi 92.40 kwa kila hisa kwa wanahisa wote waliokuwemo kwenye rejesta kufikia tarehe 3 Julai 2025.

8.4 Wanahisa walipokea na kulizingatia pendekezo la Bodi ya Wakurugenzi la malipo ya gawio la Shilingi 92.40 kwa kila hisa na wakaliidhinisha kwa utekelezaji kuanzia tarehe 15 Agosti 2025 na kuendelea.

## 9.0 UTEUZI WA MKAGUZI WA NJE WA HESABU ZA FEDHA

9.1 ILIRIPOTIWA kwamba PricewaterhouseCoopers (PwC) amekuwa Mkaguzi wa Nje wa Benki kwa kipindi cha miaka mitatu, ambapo muda wao ulimalizika tarehe 31 Desemba 2024, hivyo kulikuwa na ulazima wa kuteua Mkaguzi mwingine wa Nje kwa kipindi cha miaka mitatu.

9.2 ILIRIPOTIWA kwamba Kanuni za Benki na Taasisi za Fedha (Wakaguzi wa Nje) za mwaka 2014 zinaruhusu Mkaguzi wa Nje huyo huyo kukagua Benki moja kwa muda usiozidi vipindi viwili mfululizo, ambapo kila kipindi ni cha miaka mitatu.

9.3 ILIRIPOTIWA kwamba mchakato wa uteuzi wa Wakaguzi wa Nje ulifanyika kupitia zabuni ya ushindani ambapo KPMG Tanzania, PwC na Ernst & Young waliwasilisha zabuni zao kwa ajili ya kutoa huduma ya ukaguzi wa nje (ukaguzi wa lazima wa taarifa za fedha na ukaguzi wa TEHAMA) kwa kipindi cha miaka mitatu.

9.4 ILIRIPOTIWA kwamba baada ya kupitia zabuni zilizowasilishwa na kukamilisha mchakato wa ununuzi, Bodi ya Wakurugenzi ilipendekeza uteuzi wa Ernst & Young kuwa Wakaguzi wa Taarifa za Fedha na TEHAMA wa Benki kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2025.

9.5 ILIRIPOTIWA kwamba Wanahisa waliombwa kujadili na kuidhinisha pendekezo la Bodi ya Wakurugenzi la kuteua Ernst & Young kama Wakaguzi wa Taarifa za Fedha na TEHAMA za Benki kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2025 kwa masharti yaliyokubaliwa.

9.6 Wanahisa walipokea na kulizingatia pendekezo la Bodi ya Wakurugenzi la kuteua Ernst & Young kama Wakaguzi wapya wa Nje na wakaidhinisha utekelezaji wake.

## 10.0 UCHAGUZI WA WAKURUGENZI WA BODI

10.1 Katibu wa Kampuni aliwataarifu Wanahisa kwamba Ibara ya 80 ya Katiba ya Benki inaeleza kwamba kila baada ya miaka mitatu, theluthi moja ya Wakurugenzi hutakiwa kustaafu ukurugenzi kwenye kampuni . Kwa mujibu wa Ibara hiyo, wakurugenzi wawili yaani Bwana Robert Mtendamema na Bi. Uphoo Swai walitarajiwa kustaafu mwaka 2025 baada ya kuhudumu katika Bodi kwa vipindi viwili vya miaka mitatu kila mmoja.

10.2 ILIRIPOTIWA kwamba utaratibu wa uteuzi/uchaguzi wa Wajumbe wapya wa Bodi umeainishwa katika Ibara ya 74 ya Katiba ya Benki na Bodi ilizingatia taratibu hizo hadi kufanikisha uchaguzi wa wagombea wawili kuwa Wakurugenzi wapya wa Benki ya Biashara Mkombozi. Sifa za wagombea zilizingatia Ibara ya 76 ya Katiba ya Benki pamoja na kanuni za Benki Kuu ya Tanzania, Sheria ya Makampuni na miongozo ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana.

10.3 ILIRIPOTIWA kwamba wagombea wanne waliostahili kuchaguliwa yaani Bi Agnes Kitwanga, Bwana Damas Mugashe, Bwana Victor Tesha na Bi Susan Kyaruzi waliwasilishwa kwa Wanahisa na wakapata nafasi ya kujitambulisha na kueleza sababu za kustahili kuchaguliwa kuwa Wakurugenzi wa Benki ya Biashara Mkombozi.

10.4 ILIRIPOTIWA kwamba Wanahisa waliombwa kupiga kura na kuwachagua Wakurugenzi wawili kutoka kwenye orodha ya wagombea, ambao baadaye watapitishwa katika mchakato wa kuomba idhini ya Benki Kuu ya Tanzania kwa mujibu wa kanuni.

10.5 ILIRIPOTIWA kwamba uchaguzi wa Wakurugenzi ulifanyika na wagombea wawili walifanikiwa kuchaguliwa kuwa Wakurugenzi wapya wa Benki ya Biashara Mkombozi, yaani Bi Agnes Kitwanga na Bwana Damas Mugashe.

10.6 Mwenyekiti aliwapongeza Wakurugenzi wapya waliochaguliwa na kuwajulisha Wanahisa kwamba mchakato wa uhakiki wa uteuzi wao katika Benki Kuu ya Tanzania utaendelea kwa mujibu wa taratibu za wasimamizi.

10.7 Wanahisa walikubaliana na matokeo ya uchaguzi na wakaidhinisha uteuzi wa Bi Agnes Kitwanga na Bwana Damas Mugashe kuwa Wakurugenzi wapya wa Benki ya Biashara ya Mkombozi.

## 11.0 KUPANGA TAREHE YA MKUTANO MKUU WA MWAKA UJAO

11.1 ILIRIPOTIWA kwamba Wanahisa WALIAZIMIA kuwa Mkutano Mkuu wa Mwaka ujao ufanyike tarehe 25 Julai 2026.

## 12.0 MENGINEYO

12.1 ILIRIPOTIWA kwamba Mwenyekiti wa Bodi aliwashukuru Wanahisa kwa ushiriki na kuhudhuria mkutano.

12.2 ILIRIPOTIWA kwamba Mwenyekiti wa Bodi alimuomba Katibu wa Mkutano kusoma maazimio ya mkutano kwa ajili ya maoni na kupitishwa na Wanahisa.

12.3 ILIRIPOTIWA kwamba Katibu wa Mkutano alisoma maazimio yaliyofikiwa katikamkutano ambayo yote yaliidhinishwa na Wanahisa kama yalivyowasilishwa.

## 13.0 KUFUNGA MKUTANO

13.1 Mwenyekiti alifunga mkutano saa 15:20 alasiri.

Imethibitishwa tarehe 25 Julai 2026.

**BW. GASPER NJUU**
**MWENYEKITI**

**BI. PAULINA KUNJUMU**
**KATIBU**

# YATOKANAYO NA DONDOO ZA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA KUMI NA SITA

| S/N | MAELEKEZO YA WANAHISA AU MAOMBI YANAYOTAKIWA KUBORESHWA | HATUA ZILIZOCHUKULIWA |
|---|---|---|
| 6.1 | Kuanzisha utaratibu/dirisha katika ngazi ya matawi ambapo Wanahisa wanaweza kusahisha taarifa zao katika rejista ya wanahisa. | Benki imeanzisha dawati maalum katika Makao Makuu linalohusika na masuala ya wanahisa, likijumuisha kusahisha taarifa za Mjue Mteja Wako(KYC) kama majina, mawasiliano, namba ya CSD pamoja na taarifa za malipo. Huduma ya kusaidia wanahisa kusahisha taarifa zao pia hutolewa kupitia mtandao wa matawi ya Benki ili kuwezesha malipo ya gawio na kuhakikisha rejista ya wanahisa inabaki na taarifa sahihi na za sasa kwa rejea na kumbukumbu za baadaye. Aidha, Benki hutumia uwepo wa wanahisa wakati wa Mikutano Mikuu ya Mwaka kuthibitisha na kusahisha taarifa zao. Wanahisa pia wanaweza kusahisha taarifa zao za KYC mtandaoni kwa kujaza na kuhuisha fomu ya kielektroniki ya gawio inayotolewa na CSD and Registry Company Limited (CSDR).<br><br>Hatua hizi kwa pamoja zimeboresha kwa kiasi kikubwa usahihi na ukamilifu wa rejista ya Wanahisa. |
| 6.2 | Kurahisisha na kuboresha mchakato wa kufungua akaunti ili kuongeza usajili wa wateja utakaoleta uhamasishaji wa amana na uwekezaji. | Benki imeanzisha mfumo mpya wa kufungua akaunti ambao una muunganisho wa moja kwa moja na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) unaowezesha kufungua akaunti papo kwa papo kupitia majukwaa mbalimbali. Huduma hii tayari imetekelezwa kwenye mashine za mauzo (POS) na inasaidia usajili wa haraka wa wateja pamoja na ufunguaji wa akaunti kwa wakati mmoja.<br><br>Mpango huu umeongeza kwa kiasi kikubwa kasi ya uhamasishaji na upatikanaji wa wateja wapya kwa Benki. |

| | | |
|---|---|---|
| 6.3 | Kutumia kikamilifu fursa zilizopo katika soko maalum la Benki, hususan shule, hospitali na vyuo vinavyohusiana na Kanisa, ili kukuza biashara na utendaji wa Benki. | Benki imebuni na inaendelea kutekeleza masuluhisho mbalimbali yanayolenga kukidhi mahitaji ya taasisi mbalimbali zilizo chini ya soko lake maalum. Masuluhisho hayo yanahusisha huduma za ukwasi, uwekezaji na usimamizi wa fedha taslimu. Mpango huu umeanza kupata mafanikio mazuri na sasa Benki inaongeza kasi ya utekelezaji ili kupata sehemu kubwa zaidi ya biashara, kwa lengo la kujenga msingi endelevu wa wateja wa taasisi. |
| 6.4 | Kukamilisha utekelezaji wa miradi iliyopangwa kwa mwaka 2025. | Benki imekamilisha utekelezaji wa miradi kadhaa muhimu iliyopangwa kwa mwaka 2025, ikiwemo masuluhisho ya kidijitali ya usimamizi wa fedha taslimu kwa shule, vyuo vikuu na hospitali, zikilenga taasisi zinazomilikiwa na Kanisa kama kipaumbele kikuu.<br><br>Benki pia ipo katika hatua ya kusambaza masuluhisho hayo, ikiwa na lengo la kuandikisha jumla ya angalau shule, hospitali na vyuo 700 ifikapo mwaka 2027. Aidha, Benki ilikamilisha na kufungua tawi lake la Geita mwezi Novemba 2025, hivyo kutimiza azma yake ya kimkakati ya kujipanua na kuweka uwepo wake katika eneo hili muhimu la kiuchumi nchini. |
| 6.5 | Kuendelea kufanya ziara kwa wateja katika parokia na maeneo yenye fursa za biashara kwa ajili ya uhamasishaji wa amana, ushirikiano na ufadhili wa miradi mbalimbali. | Benki imeanzisha jukwaa la Mikutano ya Ukumbi wa Parokia ambapo hujihusisha na Uongozi wa Parokia, Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo na Viongozi wa Vyama vya Kitume kwa lengo la kuongeza uelewa wa huduma za kibenki, kufungua akaunti za benki na kuuza kwa pamoja bidhaa na huduma mbalimbali za Benki.<br><br>Mpango huu umeanza kuleta matokeo chanya katika uhamasishaji wa fursa za kibiashara za kibenki ndani ya sekta ya Kanisa. |
| 6.6 | Kufanya mapitio ya viwango vya tozo za Benki kwa kuzingatia maoni ya wanahisa kuhusu kupunguza gharama za huduma. | Benki imekagua muundo wake wa ada na tozo kwa kuzilinganisha na watoa huduma wengine wa soko ili kubaki na ushindani, huku ikizingatia muktadha wa biashara yake pamoja na mahitaji ya makundi yake lengwa ya wateja. Viwango hivyo vya tozo huchapishwa kila mwaka kwa wateja kama muongozo wa Benki kuu unavyoelekeza. |

| | | |
|---|---|---|
| 6.7 | Kuendelea kuhamasisha Kanisa na taasisi zake kutumia Benki na mifumo yake katika kufanya miamala mbalimbali. | Kanisa na taasisi zake zilizo chini ya mwamvuli wake bado ni kipaumbele chetu kikuu katika uhamasishaji wa biashara, hususan uhamasishaji wa ukusanyaji wa amana. Tunatekeleza usambazaji wa kimfumo wa masuluhisho hayo kwa kuzingatia Mkakati wetu wa Soko Maalum (Niche Market Strategy). |
| 6.8 | Kutumia majukwaa ya Kanisa kutangaza bidhaa na huduma za Benki ili kuongeza mwonekano na mwitikio wa Benki sokoni. | Benki imeendelea kutumia matukio ya Kanisa na njia za vyombo vya habari vya Kanisa ili kupenyeza huduma zake sokoni. Tunashirikiana kwa karibu na uongozi wa Kanisa pamoja na majukwaa ya vyombo vya habari kama Tumaini Media, Radio Maria, Tumaini Letu na gazeti la Kiongozi Letu ili kuwafikia hadhira pana inayojumuisha wadau wa soko maalum la Benki. |
| 6.9 | Kuimarisha uwepo wa Benki katika mikoa mbalimbali kupitia ufunguzi wa matawi na vituo vya huduma kwa kuzingatia uwezo wa mtaji na mkakati wa ukuaji. | Katika mwaka 2025, Benki ilifanikiwa kufungua tawi jipya la Geita pamoja na kuanzisha mchakato wa kujipanua katika maeneo ya Bagamoyo, Same na Kahama, ambapo Tawi la Kahama lilifunguliwa rasmi tarehe 9 Mei 2026 na Bagamoyo lilifunguliwa rasmi tarehe 6 Juni 2026.<br><br>Katika kuendelea kutathmini uwezekano wa kufungua matawi zaidi  Benki pia inatumia mtandao wake wa wakala wa kibenki kupanua huduma katika mikoa mbalimbali, pamoja na uwepo wa Wakala Mkuu maeneo mbali mbali kusaidia mtandao wa Wakala, Benki inatarajia kuendelea kupanua wigo wake wa huduma sambamba na kutathmini fursa za biashara katika maeneo lengwa. |
| 6.10 | Kuzingatia mzunguko wa maeneo ya kufanyia mkutano mkuu wa wanahisa katika mikoa muhimu kama Mwanza, Dodoma na Arusha ili kurahisisha ushiriki wa wanahisa kutoka mikoani. | Ilibainika kuwa idadi kubwa ya wanahisa na wadau wakuu wengine wanapatikana Dar es Salaam, jambo linaloipa msingi wa kuendelea kufanyika kwa Mikutano Mikuu ya Mwaka jijini Dar es Salaam. Hii pia inazingatia udogo wa Benki pamoja na uwezo wake wa kusimamia kwa uangalifu gharama zinazojitokeza ili kuimarisha na kuongeza faida kwa wanahisa. |
| 9 | Kutoa Gawio kwa faida ya mwaka 2024 | Gawio kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2024 la Shilingi 92.40 kwa kila hisa lililipwa kuanzia tarehe 15 Agosti 2025 na kuendelea,kama ilivyoamuliwa. |

| | | |
|---|---|---|
| 10 | Uchaguzi wa Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi | Benki Kuu ya Tanzania iliwapitisha na kuidhinisha uteuzi wa Bi Agnes Kitwanga na Bwana Damas Mugashe kuwa Wajumbe wapya wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya Biashara Mkombozi |



# TAARIFA YA WAKURUGENZI

## AJENDA YA 5

## 5 KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA TAARIFA YA WAKURUGENZI YA MWAKA ULIOISHIA DESEMBA 31, 2025.

### 5.1 KAZI KUU

Shughuli kuu ya Benki ni kutoa huduma za kibenki na huduma nyingine zinazohusiana, kama zilivyoainishwa katika Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 ya Tanzania. Hakukuwa na mabadiliko katika shughuli kuu za Benki katika mwaka wa fedha husika.

### 5.2 MUUNDO WA UMILIKI WA HISA

Muundo wa mtaji wa hisa unaojadiliwa ni kama ifuatavyo:

**Mtaji ulioidhinishwa**

TZS 50,000,000,000 inayojumuisha hisa 50,000,000 hisa za kawaida zenye thamani

**Hisa zilizolipiwa**

TZS 22,820,069,500 inayojumuisha hisa za kawaida 23,555,002 kila hisa ikiwa na thamani ya TZS 1,000/=. Sehemu ya hisa hizi zilizotolewa kwa punguzo kama ilivyoonyeshwa katika taarifa ya maelezo **nambari 35** ya taarifa za kifedha.

### 5.3 UMILIKI WA HISA

**HADI KUFIKIA 31 DECEMBA, 2025, UMILIKI WA HISA ULIKUWA KAMA IFUATAVYO:**

| WAMILIKI | IDADI YA HISA | THAMANI (TZS) | % YA UMILIKI |
|---|---|---|---|
| Dayosisi za Kanisa la Katoliki na taasisi zake | 7,049,049 | 6,731,213,750 | 29.50% |
| Taasisi nyingine | 2,235,141 | 2,207,832,500 | 9.67% |
| Baraza la Maaskofu wa Kanisa Katoliki Tanzania (TEC) | 4,133,995 | 4,133,995,000 | 18.12% |
| Watu Binafsi | 10,136,817 | 9,747,028,250 | 42.71% |
| **Jumla** | 23,555,002 | 22,820,069,500 | 100.0% |

## HADI 31 DESEMBA, 2024 UMILIKI WA HISA ULIKUWA KAMA IFUATAVYO:

| WAMILIKI | IDADI YA HISA | THAMANI YA HISA (TZS) | % YA UMILIKI |
|---|---|---|---|
| Dayosisi za Kanisa la Katoliki na taasisi zake | 7,049,049 | 6,731,213,750 | 29.50% |
| Taasisi nyingine | 2,235,141 | 2,207,832,500 | 9.67% |
| Baraza la Maaskofu wa Kanisa Katoliki Tanzania (TEC) | 4,133,995 | 4,133,995,000 | 18.12% |
| Watu Binafsi | 10,136,817 | 9,747,028,250 | 42.71% |
| **Jumla** | 23,555,002 | 22,820,069,500 | 100.0% |

## 5.4 WAKURUGENZI

Wakurugenzi wa Benki waliokuwa katika nafasi zao katika kipindi cha mwaka husika na hadi tarehe ya ripoti hii walikuwa:

| Jina | Wadhifa | Umri | Taaluma/Sifa | Utaifa | Tarehe ya Uteuzi/ Kustaafu |
|---|---|---|---|---|---|
| Bw. Gasper Njuu | Mwenyekiti | Miaka 66 | Diploma ya Juu ya Benki, Stashahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Fedha, Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara (MBA) Kimataifa | Mtanzania | Aliteuliwa Januari 27, 2022 |
| Bw. Respige Kimati | Mkurugenzi Mtendaji | Miaka 52 | Shahada ya Biashara katika Fedha, Shahada ya Uzamili (MSc) katika Fedha | Mtanzania | Aliteuliwa Januari 18, 2020 |
| Askofu Beatus Kinyaiya | Mjumbe wa Bodi | Miaka 69 | Askofu Mkuu Dayosisi ya Dodoma, Shahada ya Uzamili katika Historia, Shahada ya Jiografia, Shahada ya Theolojia | Mtanzania | Aliteuliwa tena 30 Mei, 2015 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Bw. Martin Mdoe | Mjumbe wa Bodi | Miaka 55 | Wakili wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Shahada ya Sheria (LLB), Shahada ya Juu ya Sheria (LLM) na Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara (MBA). | Mtanzania | Aliteuliwa Januari 27, 2022 |
| Bw. Robert Mtenda-mema | Mjumbe wa Bodi | Miaka 53 | Shahada ya Sayansi ya Kompyuta na Shahada ya Uzamili ya Sayansi Mifumo ya Mawasiliano ya Data. | Mtanzania | Aliteuliwa 8 Agosti, 2018 na alistaafu 26 Julai 2025 |
| Bi. Uphoo Swai | Mjumbe wa Bodi | Miaka 54 | Mhasibu wa Umma Aliyeidhinishwa (CPA), Diploma ya Juu ya Uhasibu, Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara. | Mtanzania | Aliteuliwa Agosti 8, 2018 na kustaafu 26 Julai, 2025 |
| Bw. Benedict Sudi | Mjumbe wa Bodi | Miaka 58 | Mhasibu wa Umma Aliyeidhinishwa (CPA), Diploma ya Juu ya Uhasibu. | Mtanzania | Aliteuliwa Mei 9, 2019 |
| Padri. Dk. Charles Kitima | Mjumbe wa Bodi | Miaka 61 | Shahada ya Sanaa katika Theolojia, Leseni katika Sheria za Canon na Shahada ya Uzamivu ya Sheria. | Mtanzania | Aliteuliwa Januari 2, 2019 |
| Bi Agnes Kitwanga | Mjumbe wa Bodi | Miaka 43 | Shahada ya Sayansi ya Kompyuta (BSc), Shahada ya Uzamili ya Mifumo ya Taarifa za Biashara (MSc). | Mtanzania | Aliteuliwa Julai 26, 2025 |
| Bw. Damas Mugashe | Mjumbe wa Bodi | Miaka 57 | Stashahada ya Juu ya Uhasibu, Stashahada ya Uzamili (PGD) katika Usimamizi wa Fedha, Shahada ya Uzamili ya Utawala wa Biashara (MBA). | Mtanzania | Aliteuliwa Julai 26, 2025. |

Wakurugenzi wafuatao wanamiliki hisa hadi kufikia mwaka huu:

| Jina la Mkurugenzi | Idadi ya Hisa | |
|---|---|---|
| | 2025 | 2024 |
| Askofu Mkuu Beatus Kinyaiya | 13,574 | 13,574 |
| Bw. Robert Mtendamema | 1,190 | 1,190 |
| Bw. Respige Kimati | 260 | 260 |
| | | |
| **Jumla ya Hisa zinazomilikiwa na Wakurugenzi** | **15,024** | **15,024** |

Hakuna mkurugenzi aliyemiliki zaidi ya asilimia 0.1 ya hisa za mtaji zilizotolewa na Benki

## 5.5 KATIBU WA KAMPUNI

Hadi kufikia Desemba 2025**,** Katibu wa Kampuni alikua ni Bi. Paulina Kunjumu.

## 5.6 UTAWALA WA SHIRIKA/KAMPUNI

Bodi ya Wakurugenzi ("Bodi") inaundwa na wakurugenzi wanane, akiwemo Mkurugenzi Mtendaji. Isipokuwa Mkurugenzi Mtendaji, hakuna mkurugenzi mwingine aliye katika nafasi ya utendaji ndani ya Benki.

Bodi ina jukumu la jumla la usimamizi wa Benki. Majukumu yake makuu ni pamoja na kubaini maeneo muhimu ya hatari, kuzingatia na kufuatilia maamuzi ya uwekezaji, kupitia masuala muhimu ya kifedha, pamoja na kutathmini utekelezaji wa mipango ya biashara na bajeti dhidi ya utendaji halisi wa Menejimenti.

Pia, Bodi inawajibika kuhakikisha kuwa Benki ina mfumo imara wa udhibiti wa ndani unaojumuisha sera na taratibu zinazofuata misingi ya utawala bora wa shirika.Kwa mujibu wa taratibu zake, Bodi hukutana angalau mara nne kwa mwaka. Hata hivyo, usimamizi wa shughuli za kila siku za Benki hukabidhiwa kwa Mkurugenzi Mtendaji, ambaye husaidiwa na Timu ya Menejimenti.

Timu ya Menejimenti hualikwa kuhudhuria vikao vya Bodi na ina jukumu la kuratibisha usimamizi wa shughuli za kila siku, sambamba na kuwa kiungo cha mawasiliano na uratibu kati ya vitengo mbalimbali vya biashara ndani ya Benki.

Katika mwaka husika, Bodi ilifanya vikao vinne vya kawaida na vikao sita vya dharura vilivyotokana na masuala maalum yaliyohitaji maamuzi ya Bodi. Muhtasari wa vikao hivyo ni kama ifuatavyo:

| Na. | Jina la Mkurugenzi | Wadhifa | Idadi ya Mikutano | Mikutano aliyohudhuria | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Gasper Njuu | Mwenyekiti wa Bodi | 10 | 10 | 100% |
| 2. | Askofu Beatus Kinyaiya | Mjumbe wa Bodi | 10 | 10 | 100 % |
| 3. | Bw. Benedict Sudi | Mjumbe wa Bodi | 10 | 10 | 100% |
| 4. | Bw. Robert Mtendamema | Mjumbe wa Bodi | 10 | 8 | 80% |
| 5. | Bi. Uphoo Swai | Mjumbe wa Bodi | 10 | 5 | 50% |
| 6. | Padre Dkt. Charles Kitima | Mjumbe wa Bodi | 10 | 8 | 80% |
| 7. | Bw. Respige Kimati | Mjumbe wa Bodi | 10 | 10 | 100% |
| 8. | Bw. Martin Mdoe | Mjumbe wa Bodi | 10 | 10 | 100% |
| 9. | Bi. Agnes Kitwanga | Mjumbe wa Bodi | 1 | 1 | 100% |
| 10. | Bw. Damas Mugashe | Mjumbe wa Bodi | 1 | 1 | 100% |

* Wakurugenzi Uphoo Swai na Robert Mtendamema walistaafu tarehe 26 Julai 2025 na nafasi zao zilichukuliwa na wakurugenzi Damas Mugashe na Agnes Kitwanga.

Bodi ina kamati tatu, ambazo ni Kamati ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vihatarishi, Kamati ya Rasilimali Watu na Uendeshaji, na Kamati ya Mikopo. Kila kamati ina kanuni elekezi zinazoongoza majukumu na wajibu wake, pamoja na kusaidia kuongeza ufanisi na tija ya utendaji wa Bodi.

Benki imejikita katika misingi ya utawala bora wa shirika, ikitambua umuhimu wa uadilifu, uwazi na uwajibikaji. Bodi ilifanya usimamizi wa karibu wa shughuli za Benki na kuhakikisha viwango vya juu vya utawala bora vinazingatiwa kupitia kamati zake kama ilivyooneshwa hapa chini:

### Kamati ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vihatarishi inaundwa na wajumbe wafuatao:

| Na. | Jina la Mkrugenzi | Wadhifa | Idadi ya Mikutano | Mikutano aliyohudhuria | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bi. Uphoo Swai | Mwenyekiti mstaafu | 6 | 4 | 67% |
| 2. | Askofu Beatus Kinyaiya | Mjumbe | 6 | 6 | 100% |
| 3. | Bw. Benedict Sudi | Mwenyekiti Mpya | 6 | 6 | 100% |
| 4 | Bw. Damas Mugashe | Mjumbe | 3 | 3 | 100% |

* Mkurugenzi Uphoo Swai alistaafu tarehe 26 Julai 2025 na nafasi yake kuchukuliwa na Mkurugenzi Damas Mugashe. Mkurugenzi Damas Mugashe alihudhuria vikao vya Bodi kuanzia Septemba 2025 hadi mwisho wa mwaka.

### Kamati ya Mikopo ya Bodi inaundwa na wajumbe wafuatao:

| Na. | Jina la Mkurugenzi | Wadhifa | Idadi ya Mikutano | Mikutano aliyohudhuria | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Robert Mtendamema | Mwenyekiti Mstaafu | 20 | 20 | 100% |
| 2. | Bw. Martin Mdoe | Mjumbe | 25 | 25 | 100% |
| 3. | Padre Dkt. Charles Kitima | Mjumbe | 25 | 20 | 80% |
| 4. | Bi. Agnes Kitwanga | Mwenyekiti Mpya | 5 | 5 | 100% |

* Mkurugenzi Robert Mtendamema alistaafu tarehe 26 Julai 2025 na alihudhuria vikao vya Bodi hadi tarehe ya kustaafu kwake. Mkurugenzi Agnes Kitwanga aliteuliwa tarehe 26 Julai 2025 na alihudhuria vikao vya Bodi kuanzia Septemba 2025 hadi mwisho wa mwaka.

### Kamati ya Rasilimali Watu na Uendeshaji inaundwa na wajumbe wafuatao:

| Na. | Jina la Mkurugenzi | Wadhifa | Idadi ya | | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Martin Mdoe | Mwenyekiti | 7 | 7 | 100% |
| 2. | Bw. Robert Mtendamema | Mjumbe Mstaafu | 7 | 5 | 71% |
| 3. | Padre Dkt. Charles Kitima | Mjumbe | 7 | 6 | 86% |
| 4. | Bi. Agnes Kitwanga | Mjumbe | 2 | 2 | 100% |

* Mkurugenzi Robert Mtendamema alistaafu tarehe 26 Julai 2025, na Mkurugenzi Agnes Kitwanga aliteuliwa kuchukua nafasi yake. Mkurugenzi Agness Kitwanga alihudhuria vikao vya Bodi kuanzia Septemba 2025 hadi mwisho wa mwaka.

### 5.7 TIMU YA UONGOZI

Mkurugenzi Mtendaji alisaidiwa na timu ya Uongozi ambao ni Wakuu wa idara mbalimbali kama afuatavyo:

| | |
|---|---|
| • Mkuu wa Idara ya Hazina<br>• Mkuu wa Idara ya Mikopo<br>• Mkaguzi Mkuu wa Ndani<br>• Afisa Mkuu wa Biashara | • Afisa Mwendeshaji Mkuu<br>• Afisa Mkuu wa Fedha<br>• Mkuu wa Idara ya Sheria (Katibu wa Kampuni)<br>• Mkuu wa Idara ya Ukubalifu na Vihatarishi |

### 5.8 HALI YA KIFEDHA YA BENKI

Benki ilipata faida kabla ya kodi ya TZS milioni 17,002 kwa mwaka ulioishia 31 Desemba 2025 (2024: TZS milioni 11,493), matokeo yaliyotokana na viashiria vifuatavyo vya utendaji:

- Mapato halisi ya uendeshaji yaliongezeka hadi TZS milioni 36,789 kutoka TZS milioni 29,216 mwaka 2024. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na ongezeko la TZS milioni 7,827 (26%) la mapato ya riba, likisaidiwa na mizania thabiti ya kifedha.

- Amana za wateja ziliongezeka hadi TZS milioni 242,862 kutoka TZS milioni 217,491 mwaka 2024, sawa na ukuaji wa 12% mwaka 2025. Ukuaji huo ulitokana na juhudi za kuhamasisha amana pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya kibenki, hususan njia za kidijitali.

- Jumla ya mali za benki ziliongezeka hadi TZS milioni 318,231 kutoka TZS milioni 282,380 mwaka 2024, hasa kutokana na ongezeko la TZS milioni 34,000 la mikopo kwa wateja na benki nyingine. Hali hii inaonyesha kuimarika kwa uwezo wa utoaji mikopo na kuongezeka kwa wigo wa wateja.

- Gharama za uendeshaji ziliongezeka hadi TZS milioni 19,786 kutoka TZS milioni 17,723 mwaka 2024, sawa na ongezeko la 12%. Ongezeko hili linatokana na upanuzi wa shughuli za biashara na kuongezeka kwa shughuli za kiutendaji.

- Jumla ya Mikopo na Karadha iliongezeka hadi TZS milioni 188,931 (2024: TZS milioni 162,565), ikiwa ni ukuaji wa 16% mwaka 2025. Ukuaji huu unaonesha ufanisi katika michakato ya utoaji mikopo na ongezeko la ushiriki wa wateja.

### Vipimo muhimu vya ufanisi wa Benki ni kama inavyoonekana hapa chini:

| Kipimo cha Ufanisi | Maana halisi ya Kipimo cha Ufanisi na ukokotoaji wake | 2025 | 2024 |
|---|---|---|---|
| Faida katika hisa | Faida kabla ya kodi/Jumla ya hisa | 34% | 29% |
| Faida katika mali | Faida kabla ya kodi/Jumla ya mali | 5% | 4% |
| Uwiano wa Gharama kwa Mapato | Gharama za uendeshaji/Faida ya riba + Mapato yasiyo ya riba | 52% | 57% |
| Faida ya riba kwenye mali zinazozalisha mapato | Jumla ya mapato ya riba/ (riba kwenye amana za serikali + salio na benki nyingine + mikopo ya benki nyingine + uwekezaji kwenye amana nyingine + mikopo halisi | 13% | 13% |
| Mapato yasiyo ya riba kwa Mapato ya Jumla | Mapato yasiyo ya riba/Jumla ya mapato | 23% | 22% |
| Faida kwa kila hisa | Faida ya Msingi/ Idadi ya Hisa za Kawaida Zilizotolewa (TZS) | 486 | 384 |
| Mikopo ghafi kwa Amana za wateja | Jumla ya mikopo na karadha kwa wateja/ Amana zote za wateja zilizopo | 78% | 75% |
| Mikopo Chechefu kwa Jumla ya mikopo ghafi | Mikopo chechefu/Mikopo yote ghafi | 4.4% | 3.8% |
| Mali zinazozalisha faida kwa Jumla ya mali | Mali zinazozalisha faida/Mali zote | 85% | 81% |
| Ongezeko la Mali | Mwelekeo (Jumla ya Mali kwa Mwaka 2025 – Jumla ya Mali kwa Mwaka 2024)/(Jumla ya Mali kwa Mwaka 2024) | 13% | 10% |

### Utoshelevu wa Mtaji

| Kipimo cha Ufanisi | Maana halisi ya Kipimo cha Ufanisi na ukokotoaji wake | 2025 | 2024 |
|---|---|---|---|
| Uwiano wa mtaji wa msingi kwa Benki za Daraja la kwanza | Mtaji wa msingi/Jumla ya mali zinazopaswa kuwepo kwa kuendana na ukubwa wa vihatarishi vilivyopo kwa mujibu wa taarifa ya hali ya kifedha, Vihatarishi katika uendeshaji na vya [vihatarishi] vilivyopo sokoni] x 100 | 20.62% | 16.93% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jumla ya uwiano wa mtaji (Daraja la 1 + Daraja la 2) | [Jumla ya Mtaji/ Jumla ya mali zinazopaswa kuwepo kwa kuendana na ukubwa wa vihatarishi vilivyopo kwa mujibu wa taarifa ya hali ya kifedha, Vihatarishi vya uendeshaji na vihatarishi vya soko] x 100 | 21.88% | 18.23% |

Mtaji msingi (Core Capital) na jumla ya mtaji (Total Capital) vilifikia TZS milioni 43,942 na TZS milioni 46,642, sawa na uwiano wa 20.62% na 21.88% mtawalia (2024: TZS milioni 35,319 na TZS milioni 38,019, sawa na 16.93% na 18.23%).

Matokeo ya mwaka huu yako juu ya masharti ya chini ya udhibiti yaliyowekwa na mamlaka, ambayo ni TZS milioni 15,000 pamoja na viwango vya chini vya 12.5% kwa mtaji msingi na 14.5% kwa mtaji jumla. Wakurugenzi wanathibitisha kuwa viwango vinavyotumika vya mahesabu vimezingatiwa na kwamba taarifa za kifedha zimeandaliwa kulingana na msingi sahihi kibiashara.

## 5.9 MTANDAO WA MATAWI

Benki ilikuwa na matawi 14 kufikia tarehe 31 Desemba 2025; manne yakiwa Dar es Salaam, mawili Mwanza, na mengine moja moja katika Bukoba, Morogoro, Dodoma, Iringa, Njombe, Moshi, Geita na Arusha.

Idadi ya jumla ya wateja wa amana na wakopaji wa Benki kufikia mwisho wa kila mwaka husika ilikuwa kama inavyoonyeshwa hapa chini:

| | 2025 | 2024 |
|---|---|---|
| **Aina ya Akaunti** | | |
| Akaunti za Hundi | 6,910 | 6,335 |
| Akaunti za Akiba | 155,872 | 166,276 |
| Akiba za muda maalum | 632 | 844 |
| **Jumla ya Akaunti** | **163,412** | **173,455** |
| **Mikopo kwa Akaunti za wateja** | **10,643** | **12,143** |

## 5.10 GAWIO

Kampuni ilipata faida halisi ya TZS milioni 11,450 (2024: TZS milioni 9,041). Katika mwaka husika, Benki ililipa gawio la TZS milioni 2,203 (2023: hakuna).

### 5.11 MATUKIO MUHIMU YALIYOTOKEA MWAKA HUU

Katika mwaka 2025, Benki iliimarisha utekelezaji wa mikakati yake kwa kuzingatia maeneo yafuatayo ya fursa:

1. Ilizindua suluhisho la usimamizi wa fedha taslimu (cash management solution) kwa shule na hospitali, ikilenga kuongeza amana na mapato yatokanayo na miamala.

2. Ilipanua mtandao wa matawi kwa kufungua tawi jipya kamili Geita, na hivyo kufikisha jumla ya matawi 14. Aidha, ilikamilisha maandalizi ya awali ya matawi matatu mapya yatakayofunguliwa Kahama, Bagamoyo na Same mwaka 2026.

3. Ilianzisha mpango mkakati maalumu kwa wateja wote wenye akaunti na benki (Account Planning Program) unaolenga kupata biashara kubwa kutoka kwao kwa lengo la kuongeza sehemu ya huduma wanazotumia benki (wallet share) kupitia mauzo ya ziada na huduma zinazokamilishana (cross-sell) pamoja na kuimarisha mnyororo wa thamani ili kupanua mizania ya benki.

4. Imeimarisha mkakati wa kuvutia na kuhudumia wateja wetu wa kimkakati( niche market) kwa kutumia suluhisho za kidijitali pamoja na bidhaa/huduma zilizoboreshwa kulenga mahitaji ya wateja wetu.

### 5.12 MIAMALA NA MIZANIA ZA WATU/TAASISI ZILIZO NA UKARIBU NA BENKI (WABIA)

Miamala yote na mizania inayohusiana na taasisi/watu waliokaribu (Wabia) na benki zimewekwa wazi katika kipengele cha 38 cha Taarifa za Fedha.

### 5.13 MAENDELEO YALIYOPANGWA

Benki inaendelea kuzingatia mipango yake mikuu ya kimkakati kwa muda mfupi na wa kati ili kufikia viwango vya faida endelevu vinavyohitajika kwa ukuaji na kurejesha gawio kwa wanahisa. Tutazingatia kuongeza idadi ya wateja kwa kuleta huduma za kibenki zenye ushindani pamoja na kutumia uwezo kamili wa wateja wetu waliopo hasa katika soko letu maalum.

## 5.14 RASILIMALI WATU

Benki ina wafanyakazi wa kutosha wenye ujuzi na uzoefu wakutosha katika nafasi muhimu za kusimamia shughuli za kibenki na kukidhi malengo ya biashara.

## 5.15 VIHATARISHI VIKUU NA MAMBO YANAYOLETA WASIWASI

### Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi

Usimamizi wa vihatarishi ni msingi wa shughuli za Benki. Vihatarishi vikuu vinavyokabili Benki vinatokana na utoaji wa mikopo kupitia shughuli zake za biashara na ukopeshaji. Aidha, Benki inakabiliwa na vihatarishi vingine kama vile vya soko, ukwasi, vya kiutendaji, sifa na nyinginezo vinavyotokana na mkakati wake, aina ya bidhaa na wigo wa shughuli zake kijiografia. Usimamizi madhubuti wa vihatarishi ni muhimu ili kuhakikisha faida endelevu, na hivyo ni sehemu muhimu ya usimamizi wa kifedha na kiutendaji wa Benki.

### Usimamizi wa Vihatarishi

Bodi ya Wakurugenzi ina jukumu la mwisho la kuweka kiwango cha vihatarishi vinavyokubalika na kuhakikisha usimamizi madhubuti wa vihatarishi. Kwa mamlaka iliyokasimiwa na Bodi, Kamati ya Bodi ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vihatarishi, husimamia na kupitia vihatarishi vya kiutendaji, vikiwemo mikopo, soko, mtaji na ukwasi.

Kamati hii pia hupitia kiwango cha vihatarishi vya Benki na kutoa mapendekezo kwa Bodi. Majukumu yake ni pamoja na kupitia ufanisi wa mifumo ya usimamizi wa hatari na udhibiti wa ndani, kuzingatia athari za mabadiliko ya kikanuni, na kuhakikisha uchambuzi wa kina katika miamala muhimu. Kamati ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vihatarishi hupokea na kuchambua taarifa za mara kwa mara kuhusu vihatarishi, sera, majaribio ya msukosuko, ukwasi na utoshelevu wa mtaji, na ina mamlaka ya kuomba taarifa yoyote ndani ya eneo lake la wajibu.

Bodi inabaki na jukumu la mwisho la mifumo ya usimamizi wa vihatarishi na udhibiti wa ndani. Wakurugenzi wanahakikisha kuwa mifumo ya udhibiti wa kifedha na kiutendaji inasimikwa na kudumishwa mara kwa mara. Ingawa hakuna mfumo unaoweza kutoa uhakika kamili dhidi ya makosa au hasara, mfumo uliopo umeundwa kutoa uhakika wa kutosha kuwa taratibu zinafanya kazi ipasavyo. Bodi ilikagua mifumo ya udhibiti wa ndani kwa mwaka ulioishia 31 Desemba 2025 na ikaona kuwa ilikidhi viwango vinavyokubalika. Tathmini hizi hufanyika kupitia Kamati ya Ukaguzi na Usimamizi was Vihatarishi ya Bodi.

### Utamaduni wa kusimamia vihatarishi

Benki inatambua kuwa watu wake ndio nguzo muhimu katika kujenga utamaduni imara wa usimamizi wa vihatarishi. Kwa hiyo, inaendelea kuwekeza katika mafunzo na maendeleo ya watumishi ili kuimarisha uelewa na utekelezaji wa taratibu za usimamizi wake.

### Usimamizi wa vihatarishi unatekelezwa kupitia mfumo wa Ngazi tatu za Ulinzi:

**Ngazi ya Kwanza ya Ulinzi:** Hii inajumuisha usimamizi na udhibiti wa ndani; mameneja wa operesheni wanamiliki na kusimamia vihatarishi. Pia, wanawajibika kutekeleza hatua za marekebisho kushughulikia kasoro za mchakato na udhibiti.

**Ngazi ya Pili ya Ulinzi:** Hiki ni kitengo huru cha usimamizi wa vihatarishi kinachohakikisha vihatarishi vinabaki ndani ya viwango vilivyokubaliwa na Benki.

**Ngazi ya Tatu ya Ulinzi:** Hii inahusisha Idara ya Ukaguzi wa Ndani inayotoa uhakiki huru na kuripoti kwa Kamati ya Ukaguzi  na Usimamizi wa Vihatarishi ya Bodi.

Maelezo zaidi ya vihatarishi vya kifedha yanapatikana katika taarifa za kifedha.

## 5.16 USIMAMIZI WA VIHATARISHI NA UDHIBITI WA MIFUMO YA NDANI

Bodi huwajibika na usimamizi wa vihatarishi na mifumo ya udhibiti wa ndani ya Benki. Ni jukumu la wakurugenzi kuhakikisha kwamba mifumo ya udhibiti wa kifedha na utendaji wa ndani imetengenezwa na kudumishwa kwa msingi wa kuendelea ili kutoa uhakika unaoridhisha kuhusiana na:

- Ufanisi katika utendaji;
- Kulinda Mali za Benki;
- Kuzingatia Sheria na Kanuni zilizopo;
- Kuaminika kwa taarifa za kihasibu;
- Muendelezo wa biashara kwa nyakati za kawaida na [nyakati] mbaya; na
- Tabia yenye kuwajibika kwa wadau wote.

Ufanisi wowote wa mfumo wa udhibiti wa ndani unategemea kufuata kwa karibu hatua zilizopendekezwa. Mara zote huwepo na hatari ya wafanyakazi kutofuata hatua hizo. Ingawa hakuna mfumo wa udhibiti wa ndani unaoweza kutoa uhakika kamili dhidi ya makosa au hasara, mfumo wa Benki umeundwa kwa namna ambayo unaipa Bodi uhakika wa kiasi kwamba taratibu zilizopo zinafanya kazi kwa ufanisi. Bodi ilipitia

mifumo ya udhibiti wa ndani kote katika mwaka wa kifedha na ina maoni kwamba zipo ndani ya vigezo vilivyokubaliwa. Bodi inachunguza ufanisi wa vihatarishi na udhibiti wa ndani kupitia Kamati ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vihatarishi na Kamati ya Mikopo ya Bodi.

## 5.17 UENDELEVU NA UONGOZI WA MAZINGIRA, [MAZINGIRA, JAMII NA UTAWALA BORA]

Utoaji wa taarifa za uendelevu wa Benki bado uko katika hatua za awali za utekelezaji. Katika kipindi hiki cha taarifa, Benki imeweka kipaumbele katika kuanzisha misingi ya utawala na nidhamu ya utoaji taarifa. Hivyo, baadhi ya maelezo bado yanatolewa kwa namna ya kiufafanuzi, kutokana na mifumo ya data, mbinu za uchambuzi na uwezo wa kitaaluma kuwa bado unaendelea kuimarishwa.

Katika hatua hii ya maendeleo, masuala ya uendelevu na yale yanayohusiana na mabadiliko ya hali ya hewa hayajapangiliwa rasmi kama ajenda huru katika vikao vya Bodi au kamati zake. Badala yake, yanashughulikiwa kupitia mfumo uliopo wa utawala wa Benki, ambapo kwa hatua kwa hatua yanaendelea kuingizwa katika usimamizi wa vihatarishi vya taasisi, utawala wa mikopo, usimamizi wa rasilimali watu na usimamizi wa uthabiti wa kiutendaji.

Kwa kuzingatia kiwango hiki cha maendeleo, masuala ya uendelevu na hali ya hewa bado hayajajumuishwa katika mifumo rasmi ya malipo yanayohusishwa na utendaji kwa Wakurugenzi au Menejimenti. Benki itafanya tathmini kwa muda kuhusu iwapo na kwa namna gani malengo ya uendelevu yanaweza kujumuishwa katika mifumo ya usimamizi wa utendaji, kadri uwezo wa ndani na mifumo ya utoaji taarifa inavyoendelea kukua.

Benki pia inapanga kujumuisha taarifa za uendelevu na masuala ya hali ya hewa katika ratiba za kawaida za taarifa za utawala kadri mifumo yake ya utoaji taarifa itakavyokomaa.

## 5.18 MASUALA MAKUBWA YENYE UWEZO WA KULETA MADHARA YA KIDHARURA

Ni maoni ya Bodi ya Wakurugenzi kwamba hakuna jambo kubwa lenye uwezo wa kuleta madhara kwa utendaji wa Benki.

## 5.19 MAZINGIRA YA WAFANYAKAZI

### Uhusiano kati ya Uongozi na Wafanyakazi

Uhusiano kati ya wafanyakazi na uongozi uliendelea kuwa mzuri. Malalamiko hushughulikiwa kupitia mikutano na majadiliano. Hamasa ya kazi inaendelea kuwa nzuri na hakukuwa na malalamiko yoyote yasiyosuluhishwa kutoka kwa wafanyakazi. Kulikuwa na ushirikiano mzuri kati ya uongozi na wafanyakazi.

Benki ni mwajiri anayeheshimu usawa. Hutoa fursa sawa za ajira na kuhakikisha kuwa mtu bora anayepatikana anateuliwa kwa nafasi yoyote bila kubaguliwa kwa aina yoyote na bila kuzingatia mambo kama jinsia, hali ya ndoa, kabila, dini, na ulemavu ambao hautaathiri uwezo wa kutekeleza majukumu.

### Mafunzo

Katika kipindi cha mwaka, Benki ilitumia TZS 71.9 milioni kwa ajili ya mafunzo ya wafanyakazi (2024: TZS 63.7 milioni). Programu za mafunzo zimekuwa zikiandaliwa na kuendelezwa ili kuhakikisha wafanyakazi wanapata ujuzi unaohitajika katika ngazi zote. Wafanyakazi walipatiwa mafunzo ya kuboresha ujuzi wao na kuongeza ufanisi kazini.

### Mikopo na Mipango ya Malipo ya Watumishi

Benki inatoa mikopo kwa wafanyakazi pamoja na mikopo ya muda mfupi ya mshahara ili kuwawezesha kukidhi mahitaji yao ya kifedha na kuimarisha maendeleo yao ya kiuchumi. Mikopo hiyo hutolewa kwa masharti maalum yaliyoidhinishwa na Bodi.

### Huduma za Matibabu

Benki hugharamia matibabu kwa wafanyakazi wote pamoja na wategemezi wao wa karibu. Aidha, wafanyakazi wote wanapatiwa bima ya afya ili kuhakikisha wanapata huduma za matibabu kwa wakati.

### Mafao ya Kustaafu

Benki huchangia kwa mujibu wa sheria katika mfuko wa hifadhi ya jamii kwa ajili ya mafao ya wafanyakazi. Wajibu wa Benki katika michango hiyo ni kwa asilimia 10 ya mshahara ghafi wa mfanyakazi.

### 5.20 Usawa wa Kijinsia

Benki ni mwajiri anayetoa fursa sawa na inahakikisha usawa wa kijinsia unaofaa kati ya wafanyakazi wake. Benki ilikuwa na wafanyakazi kama ifuatavyo kulingana na jinsia:

| **Jinsia** | **2025** | **2024** |
|---|---|---|
| Kike | 87 | 93 |
| Kiume | 109 | 103 |
| **Jumla** | **196** | **196** |

### 5.21 MICHANGO YA KISIASA

Benki haikutoa mchango wa aina yoyote kwa chama chochote cha kisiasa mwaka 2025 kama ambavyo ilifanya mwaka 2024.

### 5.22 UHUSIANO NA WADAU WENGINE

Benki iliendeleza utamaduni wa kuwa na mahusiano mazuri na wadau wake wote ikiwa ni pamoja na wadhibiti wa sekta.

### 5.23 UWAJIBIKAJI KWA JAMII NA MICHANGO YA KIBINADAMU

Benki inashiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii na programu za maendeleo katika maeneo mbalimbali nchini. Michango ya hisani iliyotolewa katika kipindi cha mwaka ilifikia TZS 53.70 milioni (2024: TZS 19.48 milioni). Benki hutoa michango kwa taasisi mbalimbali, ikiwemo vituo vya kulelea watoto yatima, kama sehemu ya msaada wa elimu kwa watoto yatima.

### 5.24 MKAGUZI WA HESABU ZA BENKI

Ernst & Young alikuwa mkaguzi wa hesabu wa Benki kwa mwaka uliomalizika tarehe 31 Desemba 2025. Pendekezo la kumteua mkaguzi wa nje wa Benki kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Desemba 2025 liliidhinishwa na wanahisa katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kumi na Sita (16), ambapo iliamuliwa kwamba Ernst & Young atakuwa mkaguzi wa Benki kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2025.

Ripoti ya Wakurugenzi iliidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi tarehe 31 Machi 2026 na kusainiwa kwa niaba ya Bodi kwa mujibu wa azimio la Bodi na:

| | |
|---|---|
| **Gasper Casmir Njuu** | **Bw. Benedict Sudi** |
| **Mwenyekiti wa Bodi** | **Mjumbe wa Bodi na Mwenyekiti wa Kamati ya Bodi ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vihatarishi** |



# TAARIFA ZA MAJUKUMU YA WAKURUGENZI KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA, 2025

Kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002 na Sheria ya Benki na Taasisi za Kifedha ya mwaka 2006 ya Tanzania, Wakurugenzi wanatakiwa kuandaa taarifa za fedha kwa kila kipindi cha fedha zinazoonesha kwa haki, katika vipengele vyote muhimu, hali ya kifedha ya Benki kufikia mwisho wa mwaka wa fedha pamoja na faida au hasara kwa mwaka husika. Wakurugenzi pia wanawajibika kuhakikisha kuwa Benki inatunza kumbukumbu sahihi za uhasibu zinazoonesha kwa usahihi wa kuridhisha hali ya kifedha ya Benki. Aidha, wanawajibika kulinda mali za Benki.

Wakurugenzi wanakubali jukumu la taarifa za fedha za mwaka, ambazo zimeandaliwa kwa kutumia sera sahihi za uhasibu zikiungwa mkono na maamuzi na makadirio ya busara na ya tahadhari, kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha (IFRS) pamoja na matakwa ya Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002 na Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 ya Tanzania. Wakurugenzi wanaona kuwa taarifa hizo zinaonesha kwa haki, katika vipengele vyote muhimu, hali ya kifedha ya Benki pamoja na matokeo yake ya kifedha kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Kifedha (IFRS) na sheria husika.

Pia, Wakurugenzi wanawajibika kutunza kumbukumbu za uhasibu zinazoweza kutegemewa katika uandaaji wa taarifa za fedha, pamoja na kubuni, kutekeleza na kudumisha mifumo ya udhibiti wa ndani inayohusiana na uandaaji na uwasilishaji wa haki wa taarifa hizo ili kuhakikisha hazina makosa ya kimateriali.

Wakurugenzi wa Benki wametathmini uwezo wa Benki kuendelea kufanya kazi kama taasisi endelevu kwa kipindi kinachotarajiwa, na hawana sababu ya kuamini kuwa Benki haitakuwa endelevu katika mwaka ujao.

Taarifa za fedha ziliidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi tarehe 31 Machi 2026 na kusainiwa kwa niaba ya Bodi na:

**Bw. Gasper Njuu**
**Mwenyekiti wa Bodi**

**Bw. Benedict Sudi**
**Mjumbe na Mwenyekiti wa Kamati ya Bodi ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vihatarishi**

# TAMKO LA MKUU WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2025

Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA), kwa mamlaka iliyopewa chini ya Sheria ya Usajili wa Wakaguzi na Wahasibu (Auditors and Accountants (Registration) Act Na. 33 ya Mwaka 1972, iliyofanyiwa marekebisho na Sheria Na. 2 ya Mwaka 1995), inahitaji taarifa za fedha ziambatane na tamko la Mkuu wa Idara ya Fedha anayehusika na maandalizi ya taarifa za fedha za taasisi husika.

Ni wajibu wa Mhasibu Mtaalamu kusaidia Bodi ya Wakurugenzi kutekeleza jukumu la kuandaa taarifa za fedha zinazoonesha kwa haki na uaminifu hali halisi ya kifedha na utendaji wa taasisi, kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji was Taarifa za Fedha (IFRS) pamoja na matakwa ya Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002 na Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 ya Tanzania. Jukumu la kisheria la mwisho la uandaaji wa taarifa za fedha liko kwa Bodi ya Wakurugenzi kama ilivyoelezwa katika Taarifa ya Majukumu ya Wakurugenzi kwenye ukurasa uliopita.

Mimi, **Vitalis Constantine Michael**, kwa nafasi yangu ya Afisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya Bishara Mkombozi ninathibitisha kuwa ninawajibika kuhakikisha kuwa taarifa za fedha za mwaka uliomalizika tarehe 31 Desemba 2025 zimeandaliwa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha (IFRS), pamoja na matakwa ya Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002 na Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 ya Tanzania.

Ninathibitisha pia kuwa taarifa hizo zinaonesha kwa haki na uaminifu hali ya kifedha na matokeo ya Benki ya Biashara Mkombozi kama yalivyokuwa kufikia tarehe hiyo na kwa mwaka ulioishia 31 Desemba 2025, na kwamba zimeandaliwa kwa misingi ya kumbukumbu za kifedha zilizo sahihi na zinazotunzwa ipasavyo.

Imesainiwa na: ______________________

**VITALIS CONSTANTINE MICHAEL,**
**WADHIFA: AFISA MKUU WA FEDHA**
**NAMBA YAKE KATIKA ORODHA YA WATAALAM WALIOSAJILIWA NA BODI YA TAIFA YA WAKAGUZI NA WAHASIBU NI: ACPA 6278**
**TAREHE: 31 MACHI 2026**

## AJENDA YA 6

## KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA TAARIFA ZA FEDHA ZA BENKI KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA , 2025 NA KUPITISHA TAARIFA YA MKAGUZI WA NJE KUHUSU TAARIFA ZA FEDHA ZA BENKI KWA MWAKA ULIOSHIA TAREHE 31 DESEMBA 2025.

## MUKTASARI WA RIPOTI YA MKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA

### Maoni

Tumekagua taarifa za kifedha za Benki ya Biashara Mkombozi ("Benki") zilizopo katika kurasa 62 hadi 90. Taarifa hizo zinajumuisha Taarifa ya Hali ya Kifedha hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2025, Taarifa ya Faida au Hasara na Mapato Mengine ya kina, Taarifa ya Mabadiliko katika Mtaji, na Taarifa ya Mtiririko wa Fedha kwa mwaka uliomalizika, pamoja na maelezo ya taarifa za kifedha, ikiwemo muhtasari wa sera muhimu za uhasibu.
Maoni yetu ni kuwa Taarifa za Fedha zimetoa mtazamo wa ukweli na wa haki kuhusu hali ya kifedha ya Benki ya Biashara Mkombozi kwa mwaka ulioshia Desemba, 2025. Taarifa za utendaji wa kifedha na ya Mtiririko wa Fedha zimetolewa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya kihasibu na kulingana na matakwa ya Sheria ya Kampuni Na. 12 ya Mwaka 2002.

### Msingi wa Maoni

Tumefanya ukaguzi wetu kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISAs). Majukumu yetu chini ya viwango hivyo yamefafanuliwa zaidi katika sehemu ya ripoti yetu inayohusu majukumu ya mkaguzi katika ukaguzi wa taarifa za fedha.Tunaamini kuwa ushahidi wa ukaguzi tulioupata unatosha na unafaa kutoa msingi wa maoni yetu.

Tuko huru na Benki kwa kuzingatia Kanuni za Kimataifa za Maadili kwa Wahasibu Wataalamu (ikiwemo Viwango vya Kimataifa vya Uhuru) zilizotolewa na Bodi ya Kimataifa ya Viwango vya Maadili kwa Wahasibu (IESBA Code), pamoja na masharti ya kimaadili ya Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA) yanayotumika kwa ukaguzi wa taarifa za kifedha nchini Tanzania. Tumetekeleza majukumu yetu mengine ya kimaadili kwa mujibu wa IESBA Code na masharti ya NBAA.

## RIPOTI KUHUSU MATAKWA YA KISHERIA NA KANUNI NYINGINE

Ripoti hii, ikiwemo maoni yaliyotolewa, imeandaliwa kwa ajili ya wanachama wa Benki kama kundi moja kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni, Na. 12 ya mwaka 2002, na kwa madhumuni hayo pekee.

Kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni, Na. 12 ya mwaka 2002, tunatakiwa pia kutoa taarifa iwapo, kwa maoni yetu, ripoti ya wale walio na jukumu la utawala hailingani na taarifa za kifedha, iwapo Benki haikuweka kumbukumbu sahihi za uhasibu, iwapo taarifa za kifedha haziendani na kumbukumbu hizo, iwapo hatujapokea taarifa zote na maelezo tunayohitaji kwa ukaguzi wetu, au iwapo taarifa zinazohitajika kisheria kuhusu malipo ya wakurugenzi na miamala na Benki hazijafichuliwa. Kuhusu masharti hayo, hatuna jambo la kuripoti.

Mshirika mkuu wa ukaguzi aliyehusika na ripoti hii ya mkaguzi huru ni Dkt. Neema Kiure.

Ernst & Young

**KWA NIABA YA ERNEST AND YOUNG**
**CERTIFIED PUBLIC ACCOUNTANTS**
**DAR ES SALAAM**

**CPA DKT. NEEMA KIURE (FCPA 1227)**
**MSHIRIKA**

**TAREHE:** 31 March 2026

**NBAAVN:25FCPA1227TZH2PYLE**

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA BENKI KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2025

| | Kipe-ngele | 2025 TZS'000 | 2024 TZS'000 |
|---|---|---|---|
| Mapato ya riba yaliyokokotolewa kwa kutumia mbinu ya kiwango halisi cha riba | 8 | 35,976,572 | 30,108,219 |
| Gharama za riba zilizokokotolewa kwa kutumia mbinu ya kiwango halisi cha riba | 9 | (8,656,704) | (7,702,557) |
| **Mapato Halisi ya Riba** | | **27,319,868** | **22,405,662** |
| Hasara tarajiwa za mikopo | 10 | (1,518,154) | (1,651,387) |
| **Mapato halisi ya Riba baada ya Hasara tarajiwa za Mikopo** | | **25,801,714** | **20,754,275** |
| Mapato ya ada na kamisheni | 11 | 6,807,174 | 4,252,461 |
| Mapato Mengine | 12 | 1,439,041 | 1,405,242 |
| Faida halisi inayotokana na kuondolewa kwenye vitabu kwa mali za kifedha zilizopimwa kwa thamani ya haki kupitia mapato mengine ya kina | 23(b) | 235,134 | 159,086 |
| Mapato halisi yatokanayo na biashara ya fedha za kigeni. | 13 | 2,505,688 | 2,645,395 |
| **Jumla ya Mapato Yasiyo ya Riba** | | **10,987,037** | **8,462,184** |
| **Faida Halisi ya Uendeshaji** | | **36,788,751** | **29,216,459** |
| Matumizi ya wafanyakazi | 14 | (9,975,500) | (9,256,991) |
| Kushuka thamani kwa Mali | 15 | (2,652,564) | (2,182,975) |
| Matumizi mengine ya uendeshaji | 16 | (7,158,696) | (6,283,193) |
| **Jumla ya Matumizi ya Uendeshaji** | | **(19,786,759)** | **(17,723,159)** |
| **Faida Kabla ya Kodi ya Mapato** | | **17,001,992** | **11,493,300** |
| Tengo la Kodi ya Mapato | 17 | (5,551,175) | (2,451,883) |
| **Faida ya Mwaka** | | **11,450,817** | **9,041,417** |
| Mapato mengine yote yaliyojumuishwa | | | |
| ***Vipengele vinavyoweza kurekebishwa baadaye kwa faida au hasara*** | | | |
| FVOCI Uwekezaji katika Amana; | | | |
| - Thamani halisi ya (hasara)/faida iliyopatikana kwa mwaka kutokana na (Kipengele 23a) | | 20,558 | (273,857) |
| -Kodi yake | | (6,167) | 82,157 |
| Mapato mengine yote baada ya kutoa kodi | | **14,391** | **(191,700)** |
| **Jumla ya mapato yote kwa mwaka baada ya kodi** | | **11,465,207** | **8,849,717** |
| **Mapato kwa Kila Hisa** | | **TZS** | **TZS** |
| **Mapato kwa kila Hisa ya Msingi na Iliyopunguzwa** | **18** | **486** | **384** |

## TAARIFA YA HALI YA FEDHA YA BENKI HADI 31 DESEMBA 2025

| **MALI** | **Kipengele** | **2025**<br>**TZS '000** | **2024**<br>**TZS '000** |
|---|---|---|---|
| Fedha taslimu na akiba na Benki Kuu ya Tanzania | 19 | 25,802,786 | 23,398,540 |
| Mikopo na karadha na Benki nyingine | 20 | 30,365,679 | 22,730,935 |
| Uwekezaji katika Amana za Serikali – FVOCI | 23(a) | 1,960,069 | 10,875,000 |
| Mikopo na karadha kwa wateja | 22 | 188,931,898 | 162,565,818 |
| Kodi ya mapato ya sasa inayoweza kurejeshwa | 17 | 612,484 | 76,144 |
| Dhamana za serikali – zilizopimwa kwa gharama iliyopunguzwa | 24 | 50,926,184 | 41,538,307 |
| Mali Nyingine | 21 | 6,241,004 | 5,054,408 |
| Uwekezaji katika Hisa | 25 | 487,000 | 539,000 |
| Mali isiyohamishika na Mitambo | 28 | 5,001,623 | 5,637,947 |
| Mali za haki ya matumizi | 26 | 4,952,327 | 7,046,812 |
| Mali ya Kodi iliyoahirishwa muda wa kulipa kwake | 29 | 258,469 | 1,648,305 |
| Mali zisizoshikika (Intangible Assets) | 27 | 2,692,085 | 1,269,416 |
| **JUMLA YA MALI** | | **318,231,608** | **282,380,632** |

| **MADENI NA MTAJI (HISA)** | | | |
|---|---|---|---|
| **Madeni** | | | |
| Amana zinazodaiwa na benki nyingine | 30(a) | 11,856,257 | 9,511,626 |
| Amana zinazodaiwa na Wateja | 30(b) | 242,862,512 | 217,491,606 |
| Madeni mengine | 32 | 3,595,254 | 2,185,341 |
| Mikopo | 31(a) | 1,509,221 | 1,508,323 |
| Mikopo ya chini (Isiyopewa kipaumbele katika kulipa) | 31(b) | 3,346,962 | 3,119,721 |
| Matengo | 33 | 649,454 | 905,724 |
| Madeni ya Kukodisha | 34 | 5,062,551 | 7,570,371 |
| | | **268,882,211** | **242,292,712** |

| **MTAJI/HISA** | | | |
|---|---|---|---|
| Mtaji wa Hisa | 35 | 23,555,002 | 23,555,002 |
| Hisa zilizopunguzwa thamani | 35 | (734,932) | (734,932) |
| Mapato yaliyoliyohifadhiwa | | 22,547,511 | 14,510,180 |
| Akiba ya Kikanuni za Udhibiti | 36(a) | 4,598,346 | 3,388,590 |
| Akiba nyingine-FVOCI | 36(b) | (616,530) | (630,920) |
| | | **49,349,397** | **40,087,920** |
| **JUMLA YA MADENI NA MTAJI/HISA** | | **318,231,608** | **282,380,632** |

Idhini ya kuchapishwa kwa taarifa hizi za kifedha imetolewa na Bodi ya Wakurugenzi tarehe 31 Machi 2026, na zilitiwa saini kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi na:

| | |
|---|---|
| **BW. GASPER CASMIR NJUU**<br>**MWENYEKITI WA BODI** | **BW. BENEDICT SUDI**<br>**MJUMBE WA BODI NA MWENYEKITI WA KAMATI YA UKAGUZI NA USIMAMIZI WA VIHATARISHI** |



## TAARIFA YA MBADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA ULIOISHIA DESEMBA 31 2025

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio lililokuwepo hadi 01 Januari 2025** | **23,555,002** | **(734,932)** | **14,510,180** | **3,388,590** | **(630,920)** | **40,087,920** |
| Faida ya mwaka | - | - | 11,450,817 | - | **-** | **11,450,817** |
| Faida inayotokana na kufanya tathmini upya | - | - | - | - | 255,692 | 255,692 |
| Ongeza: Faida ya tathmini upya iliyohamishiwa kwenye faida au hasara (23(b)) | - | - | - | - | (235,134) | (235,134) |
| Mapato mengine jumla | | | | | 20,558 | **20,558** |
| Toa: Kodi yake | | | | | (6,167 | (6,167 |
| **Mapato mengine yote kwa mwaka baada ya Kodi** | | | | | **14,391** | **14,391** |
| Gawio lililolipwa | - | - | (2,203,730) | - | - | **(2,203,730)** |
| * Hamisho kutoka akiba ya Kinanuni za Udhibiti | - | - | (1,209,756) | 1,209,756 | - | - |
| **Hadi 31 Desemba 2025** | **23,555,002** | **(734,932)** | **22,547,511** | **4,598,346** | **(616,530)** | **49,349,398** |

** Akiba ya kikanuni (Regulatory reserve) ni fedha zinazotengwa kwa ajili ya kufidia nyongeza ya hasara za mikopo inayotakiwa kwa mujibu wa miongozo ya kiudhibiti ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT). Akiba hii hairuhusiwi kugawiwa kama gawio au kutumika kwa mgawanyo mwingine kwa wanahisa.

## TAARIFA YA MBADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA ULIOISHIA DESEMBA 31 2024

| | Mtaji wa Hisa TZS' 000 (Note 35) | Hisa Zilizo-punguzwa thamani TZS' 000 (Note 35) | Mapato yaliyohifa-dhiwa TZS' 000 | Akiba ya Kikanuni za Udhibiti ** TZS' 000 (Note 36(a)) | Akiba ya thamani ya haki TZS' 000 (Note 36(b)) | Total TZS' 000 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio lililokuwepo hadi 01 Januari, 2024** | **23,555,002** | **(734,932)** | **3,434,731** | **5,422,622** | **(439,220)** | **31,238,203** |
| Faida ya mwaka | - | - | 9,041,417 | - | **-** | 9,041,417 |
| Hasara inayotokana na kushuka kwa thamani ya mali baada ya kufanyiwa tathmini mpya | - | - | - | - | (114,771) | (114,771) |
| Ongeza: Faida ya tathmini upya iliyo-hamishiwa kwenye faida au hasara 23(b) | - | - | - | - | (159,086) | (159,086) |
| **Mapato mengine kwa ujumla wake** | **-** | **-** | **-** | **-** | **(273,857)** | **(273,857)** |
| Punguza Kodi yake | - | - | - | - | 82,157 | 82,157 |
| **Mapato mengine yote baada ya kodi** | **-** | **-** | **-** | **-** | **(191,700)** | **(191,700)** |
| **Mapato mengine yote kwa mwaka baa-da ya Kodi** | - | - | - | - | **(191,700)** | **(191,700)** |
| *Hamisho kutoka akiba ya Kinanuni za Udhibiti | - | - | 2,034,032 | (2,034,032) | - | - |
| **Hadi 31 Desemba 2024** | **23,555,002** | **(734,932)** | **14,510,180** | **3,388,590** | **(630,920)** | **40,087,920** |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2025

| | Kipen-gele | 2025 TZS'000 | 2024 TZS'000 |
|---|---|---|---|
| **Mtiririko wa fedha kutokana na Shughuli za Uendeshaji** | | | |
| Faida Kabla ya Kodi | | 17,001,992 | 11,493,300 |
| ***Marekebisho:*** | | | |
| Gharama za riba katika Madeni ya kukodisha | 9 | 612,896 | 737,107 |
| Hasara za mikopo zinazotarajiwa (ECL) kwenye mali za kifedha | 10 | 1,518,154 | 1,651,387 |
| Kupungua thamani kwa mali ambazo Benki inayo haki ya kuzitumia kwa muda mrefu | 15 | 1,013,328 | 1,013,984 |
| Kupungua thamani kwa mali zisizoshikika | 15 | 431,738 | 67,871 |
| Hasara itokanayo na fedha za kigeni ambazo hazijauzwa | 34 | (2,505,688) | (2,645,395) |
| Kushuka thamani kwa mali na mitambo | 15 | 1,207,497 | 1,101,120 |
| Gharama za madeni | 30(a) | 591,801 | 534,059 |
| Tengo la Mapato ya Riba kwa hesabu za Riba Yenye Maslahi | 23(b) | (235,134) | (159,086) |
| Kuongezeka/Kupungua kunakotokana na matengo | 33 | (444,847) | (408,489) |
| Mapato ya Riba | 8 | (35,976,572) | (30,108,219) |
| Gharama za riba kwenye amana za wateja | 9 | 6,842,726 | 6,138,295 |
| | | **(10,284,760)** | **(10,584,066)** |
| ***Mabadiliko katika Mali na Madeni ya Uendeshaji:*** | | | |
| Mabadiliko ya Hifadhi ya Kiwango cha chini cha Kisheria | | (1,000,632) | (435,286) |
| Mabadiliko katika Mali nyingine | | (1,186,596) | (768,821) |
| Mabadiliko katika Mikopo na Karadha kwa wateja | | (25,649,466) | (28,304,431) |
| Mabadiliko katika amana za wateja | | 25,370,906 | 10,094,796 |
| Mabadiliko katika amana zinazodaiwa na benki nyingine | | 2,344,631 | 9,511,626 |
| Malipo kwa wastaafu | | (701,117) | (231,105) |
| Mabadiliko ya madeni mengine | | 1,409,913 | (91,747) |
| **Fedha taslimu zilizopatikana katika Uendeshaji** | | **587,639** | **(10,224,968)** |
| Mapato ya Riba | | 37,738,347 | 32,736,072 |
| Gharama za Riba | | (6,548,896) | (5,944,464) |
| Kodi ya Mapato iliyolipwa | 17 | (4,697,679) | (2,890,493) |
| Marejesho ya Kodi | | - | 220,053 |
| **Fedha taslimu halisi kutoka katika Shughuli za Uendeshaji** | | **16,794,651** | **3,312,134** |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2025

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Mtiririko wa Fedha kutokana na Shughuli za uwekezaji** | | | |
| Uwekezaji katika Dhamana za Serikali – Malipo ya taratibu | | (9,387,877) | (9,057,792) |
| Uwekezaji katika Dhamana- FVOCI | | 8,914,931 | 9,500,253 |
| Ununuzi wa vifaa na mitambo | 28 | (1,571,425) | (2,070,185) |
| Ununuzi wa mali zisizoshikika | | (875,685) | (1,056,441) |
| **Fedha kutokana halisi na Shughuli za uwekezaji** | | **(2,920,056)** | **(2,684,165)** |
| | | | |
| **Mtiririko wa Fedha kutokana na Shughuli za Ufadhili** | | | |
| Deni la ukodishaji lililolipwa – La msingi | 34 | (1,490,458) | (2,026,755) |
| Malipo ya urejeshaji wa madeni ya upangaji na riba iliyolipwa | 34 | (166,880) | (212,753) |
| Riba ya madeni iliyolipwa | 31(a) | (318,142) | (140,856) |
| Malipo ya urejeshaji wa madeni ya daraja la chini | 31(b) | (63,000) | (126,000) |
| Malipo ya Gawio | | (2,203,730) | - |
| **Fedha taslimu zilizotumika katika shughuli za ufadhili** | | **(4,242,210)** | **(2,506,364)** |
| **Ongezeko/Pungozo jumla la pesa taslimu na mali zinazoweza kubadilishwa kuwa pesa kwa haraka** | | **9,632,385** | **(1,878,395)** |
| Fedha taslimu na mali zinazoweza kubadilishwa kuwa fedha kwa haraka mpaka Januari 1 | | 36,086,752 | 37,962,062 |
| Tofauti za kubadilishana fedha za kigeni | | (1,777) | 3,085 |
| **Fedha taslimu na mali zinazoweza kubadilishwa kuwa pesa hadi Desemba 31** | **37** | **45,717,360** | **36,086,752** |

## TATHMINI JUU YA KUENDELEA KWA BIASHARA YA BENKI

### 1. MSINGI WA UTAYARISHAJI

**Taarifa ya uzingatiaji na msingi wa utayarishaji**

Taarifa za kifedha za Benki zimeandaliwa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu (IFRS) vilivyotolewa na Bodi ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu (IASB), pamoja na matakwa ya Sheria ya Taasisi za Kibenki na Fedha ya mwaka 2006 na Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002 za Tanzania.

Taarifa hizi zimeandaliwa kwa msingi wa gharama ya kihistoria, isipokuwa pale ambapo imeelezwa vingine katika sera za uhasibu. Zimewasilishwa kwa kutumia sarafu ya Tanzania (TZS), na kiasi kimeoneshwa kwa takwimu za karibu elfu (TZS'000), isipokuwa pale ambapo imeelezwa vingine.

Kwa madhumuni ya kuripoti kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002 na Sheria ya Taasisi za Kibenki na Fedha ya mwaka 2006 ya Tanzania, taarifa ya hali ya kifedha (balance sheet) imewasilishwa kama taarifa ya hali ya kifedha (statement of financial position), na taarifa ya faida au hasara imewasilishwa kama taarifa ya faida au hasara na mapato mengine ya kina.

Utayarishaji wa taarifa za kifedha kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu (IFRS) unahitaji matumizi ya makadirio muhimu ya kihasibu na uamuzi wa kitaalamu wa uongozi wa Benki na wakurugenzi katika kutumia sera za uhasibu. Mabadiliko ya makadirio au dhana yanaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa taarifa za kifedha katika kipindi husika.

Wakurugenzi wanaamini kuwa makadirio na dhana zilizotumika ni sahihi na kwamba taarifa hizi zinaonesha kwa uaminifu hali ya kifedha na matokeo ya Benki.

## 2. MSINGI WA UTAYARISHAJI (INAENDELEA)

### Uendelevu wa shughuli za Benki

Mtaji mkuu wa Benki, mtaji wote, uwiano wa mtaji mkuu na uwiano wa mtaji wote ulikuwa TZS 43,942 milioni (2024: TZS 35,319 milioni) na TZS 46,642 milioni (2024: TZS 38,019 milioni), sawa na 20.62% na 21.88% (2024: 16.93% na 18.23%). Kiwango cha mtaji mkuu na uwiano wa mtaji vyote vilikuwa ndani ya viwango vya kisheria vya chini vya TZS 15,000 milioni, pamoja na matakwa ya kikanuni ya 12.5% na 14.5% mtawalia.

Hali ya mtaji mkuu na mtaji wote wa Benki inategemea mambo kadhaa, ikiwemo matokeo ya kifedha, upatikanaji wa mtaji wa ziada wa hisa, na kiwango cha mali zenye uzito wa hatari. Wakurugenzi na Menejimenti wanatarajia kuwa hali hizi zitaendelea kuboreka.

Menejimenti na wakurugenzi wa Benki wamefanya tathmini ya uwezo wa Benki kuendelea kufanya kazi kama taasisi inayoendelea (going concern) na wamehitimisha kuwa hakuna sababu za kuamini kuwa Benki haitaweza kuendelea kufanya kazi. Hivyo, taarifa za kifedha zimeandaliwa kwa msingi wa kuendelea kwa shughuli (going concern assumption).

Hali ya ukwasi ya Benki inatarajiwa kuwa ya kutosha kukidhi madeni yanayostahili kulipwa pamoja na mahitaji mengine ya biashara, na inatarajiwa kuendelea kuwa hivyo kwa muda unaoonekana mbele.

Menejimenti na wakurugenzi wataendelea kuchukua hatua za tahadhari, ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji wa karibu wa viwango muhimu vya ukwasi, mtiririko wa fedha, usimamizi makini wa nafasi za kifedha na miamala ya kila siku, kuweka kipaumbele katika utoaji wa mikopo ili kupunguza hatari ya kushindwa kulipa na matatizo ya ukwasi, pamoja na ufuatiliaji wa kwingineko wa mikopo ili kuchukua hatua za marekebisho kwa wakati unaofaa.

## 8 MAPATO YA RIBA

| | 2025<br>TZS'000 | 2024<br>TZS'000 |
|---|---|---|
| Mapato ya riba iliyokokotolewa kwa kutumia njia ya riba halisi hujumuishwa: | | |
| Mikopo na Karadha | 28,027,285 | 22,435,612 |
| Amana za Serikali na za Kampuni | 7,359,443 | 6,872,774 |
| Uwekezaji wa fedha kwa muda mfupi | 589,844 | 799,833 |
| | **35,976,572** | **30,108,219** |

## 9. GHARAMA/MATUMIZI /YA RIBA

| | 2025<br>TZS'000 | 2024<br>TZS'000 |
|---|---|---|
| Gharama ya riba iliyokokotolewa kwa kutumia njia ya riba halisi | | |
| Amana za muda maalum | 6,001,245 | 5,811,540 |
| Amana za Akiba | 841,481 | 758,461 |
| Amana zinazotokana na benki nyingine | 591,801 | 11,626 |
| Mikopo * | 319,040 | 120,823 |
| Mkopo wa daraja la chini (Kipengele 31b) | 290,241 | 263,000 |
| Gharama ya riba kwenye madeni ya upangaji (Ki-pengele 34) | 612,896 | 737,107 |
| | **8,656,704** | **7,702,557** |

* Hii inahusiana na kukopa kutoka TMRC, rejea Kumbukumbu 31 (a)

## 10. HASARA TARAJIWA YA MADENI

| | 2025<br>TZS'000 | 2024<br>TZS'000 |
|---|---|---|
| Kuongezeka/Kupungua kwa ECL kwenye mikopo kwa wateja **(Kipengele 22)** | 1,351,368 | (506,954) |
| Amana za Serikali **(Kipengele 24)** | 179,146 | - |
| Mikopo na Karadha zilizokopeshwa kwa benki nyingine **(Kipengele 20)** | 56,560 | - |
| Utoaji wa akiba ya hasara ya mikopo inayotarajiwa (ECL) kwenye mali nyingine **(Kipengele 21)** | (68,920) | - |
| Kufuta kwenye vitabu vya uhasibu kwa mikopo mingine isiyolipika | - | 2,158,341 |
| | **1,518,154** | **1,651,387** |

## 11. MAPATO YA ADA NA KAMISHENI

| ***Mapato ya ada yanayopatikana kutokana na huduma zinazotolewa kwa muda:*** | **2025 TZS'000** | **2024 TZS'000** |
|---|---|---|
| Ada ya kuidhinishia mkopo | 1,476,819 | 1,401,713 |
| ***Mapato ya ada kutokana na kutoa huduma za kifedha kwa wakati fulani:*** | | |
| Gharama za huduma | 962,974 | 557,385 |
| Ada ya huduma za kutoa fedha | 372,124 | 363,447 |
| Kamisheni itokanayo na huduma ya kuhamisha fedha kwa njia ya Western Union | 12,445 | 19,428 |
| Kamisheni itokanayo na huduma za kuhamisha fedha | 143,481 | 26,324 |
| Kamisheni itokanayo na tozo za huduma ya kutoa fedha kwa Commission on ATM | 142,286 | 158,338 |
| Ada za Mawakala wa Benki huduma za kibenki kwa njia ya simu za mkononi | 441,756 | 376,457 |
| Kamisheni ya huduma za Bima | 626,341 | 527,998 |
| Kutoa huduma ya dhamana ya Benki | 1,582,664 | 257,388 |
| Ada Nyinginezo* | 1,046,284 | 563,983 |
| | **6,807,174** | **4,252,461** |

* Ada nyinginezo ni pamoja na ada za malipo ya mapema ya mikopo, ada za uhaulishaji wa fedha kwenda nje, ada za huduma za benki mtandaoni, ada za utoaji wa kadi za ATM, ada za kuchakata mishahara, na ada za utoaji wa daftari la hundi.

## 12. MAPATO MENGINE

| | **2025 TZS'000** | **2024 TZS'000** |
|---|---|---|
